# TATHMINI YA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA SOMO LA IMLA KATIKA SHULE ZA UPILI: GATUZI LA TRANS-NZOIA, KENYA


**NA**

**KUREMA AOKO LONAH**

**IDARA YA KISWAHILI**


**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**OKTOBA, 2021**

i

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kingine

Sahihi__________ Tarehe 29/10/2021

Kurema Aoko Lonah

C50/CE/28517/2013

Tasnifu hii imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta

Sahihi__________ Tarehe 29/10/2021

Dkt. Miriam Osore

Idara ya Kiswahili

Sahihi__________ Tarehe 29/10/2021

Dkt. Leonard Chacha Mwita

Idara ya Kiswahili

# TABARUKU

Tasnifu hii naitabaruku kwa babangu mzazi, marehemu Anesmas Mabiala Kurema kwa kunielimisha, kunihimiza, kunifadhili na kujitolea kwa vyovyote vile kuhakikisha ndoto yangu ya elimu imetimia.

# SHUKRANI

Namshukuru Maulana kwa kunipa siha njema na kuniwezesha kukamilisha kazi hii. Ningependa kuwashukuru waelekezi wangu Dkt. Miriam Osore na Dkt. Leonard Chacha Mwita kwa kunielekeza na kunishauri hadi nilipotamatisha kazi hii. Sitasahau kuwashukuru wahadhiri wengine katika Idara ya Kiswahili kwa kuniwekea msingi dhabiti mwanzoni mwa kozi. Namshukuru mamangu mzazi Everlyne Kurema kwa kunihimiza na kuniombea kila mara hasa nilipokumbana na changamoto mbalimbali katika kazi hii. Isitoshe, nawashukuru ndugu zangu kwa kunitia moyo kila mara. Shukran jazilla kwa walimu na wanafunzi wa shule mbalimbali nilizofanyia utafiti, bila nyinyi huenda malengo ya utafiti huu hayangetimia. Mwisho, namshukuru mwanangu Adriel Baraka kwa kuvumilia upweke wa kukosa malezi ya mama kila mara niliposafiri kwa ajili ya kufanikisha masomo yangu. Mungu awabariki nyote.

# IKISIRI

Utafiti huu ulitathmini ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla katika shule za upili katika Gatuzi la Trans-Nzoia. Utafiti huu ulilenga kubainisha vipengele vya stadi ya uandishi ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla, mbinu ambazo walimu hutumia kufundishia somo la imla, changamoto zilizowakumba walimu katika ufunzaji wa imla na udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo na kupendekeza namna ya kuliboresha. Uteuzi wa sampuli kusudi ulitumiwa kuchagua gatuzi lililohusishwa katika utafiti huu. Shule zilizotafitiwa ziliteuliwa kwa kutumia sampuli tabakishi na bahatishi. Nadharia zilizoongoza utafiti huu ni Nadharia ya Lugha Mawasiliano iliyoasisiwa katika miaka ya 1960 na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967). Mihimili ya Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano ilitumiwa kuchanganua mbinu za ufundishaji wa somo la imla ilhali Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilitumiwa kudhihirisha vipengele vya stadi ya kuandika katika somo la imla na udhaifu katika ujifunzaji wa somo hilo katika shule za sekondari. Utafiti huu ulifanywa nyanjani. Mbinu za mahojiano na uchunzaji zilitumiwa kukusanya data. Data hiyo imewasilishwa kutumia maandishi ya nathari, majedwali na vielelezo. Matokeo yamebaini kuwa walimu wengi katika shule za sekondari wanafundisha somo la imla kijuujuu bila kufanya maandalizi ya kimaksudi. Aidha, utafiti huu umeonyesha kuwa wanafunzi wanajifunza vipengele mbalimbali vya lugha kama vile hijai, sarufi, hati bora, msamiati na matamshi bora katika somo la imla. Utafiti huu unapendekeza walimu waandaliwe warsha mbalimbali za Kiswahili ili wahamasishwe kuhusu mbinu mbalimbali za kufundishia somo la imla. Aidha, silabasi ya Kiswahili ifanyiwe marekebisho ili kuwezesha maandalizi ya kimaksudi ya ufundishaji wa imla. Isitoshe, utafiti huu unapendekeza tume ya kuwaajiri walimu (T.S.C) iwaajiri walimu zaidi na kuwaruhusu walimu wa Kiswahili kufundisha Kiswahili lugha na Fasihi pekee ili kuwapa walimu muda wa kutosha wa kufundisha vipengele vyote vya stadi za lugha.

## ABSTRACT

This study sought to analyze the teaching and learning of dictation in secondary schools in Trans-Nzoia County. The study had the following objectives; to identify the writing skills that students learn from dictation exercises, to identify the methods that teachers used in teaching dictation in secondary schools, to identify the problems encountred by teachers when teaching dictation and to establish the weaknesses in teaching and learning dictation and propose ways of correcting them. Purposive sampling was used to select Trans-Nzoia county which was used in the study. Schools involved in the study were selected through cluster and random sampling. Schools were put into different clusters and one school was selected randomly fom each cluster. The tenets of Theory of Language of Communication were used to analyse the different methods of teaching dictation. The Error Analysis Theory which was put forward by Corder (1967) was used to analyse the weaknesses of learning and teaching dictation and explain how they can be eliminated. This study was mainly carried out in the field. The data collection methods included interviews and class observations. The data collected has been presented in writing and tables. The study found out that secondary school teachers teach dictation without adequate preparation. The study also revealed that students learn a lot of language skills like spelling, grammar, handwriting, vocabulary and pronounciation from dictation. This study recommends that the Kiswahili syllabus should be revised so that it gives more emphasis on teaching dictation. It also recommends that teachers be inducted on methods of teaching dictation, the teachers' employer (T.S.C) to employ more Kiswahili teachers and they should be allowed to teach Kiswahili subject only without combining with another subject.

# YALIYOMO

Ungamo…………………………………………………………………………. i

Tabaruku……………………………………………………………………...ii

Shukrani……………………………………………………………………...iii

Ikisiri…………………………………………………………………...….iv

Abstract……………………………………………………………………....v

Yaliyomo…………………………………………………………………....... vi

Viambatisho………………………………………………………………… x

Orodha ya Majedwali na Vielelezo……………………………………….. xi

Orodha ya Vifupisho……………………………………………………… xii

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI**

1.0 Usuli wa Mada ………………………………………………………........1

1.1 Suala la Utafiti ………………………………………………………........6

1.2 Malengo ya Utafiti……………………………………………………………7

1.3 Maswali ya Utafiti……………………………………………………………8

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ya Utafiti ……………….……………………....8

1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti…………………………………………… 10

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada……………………………….……........11

1.7 Misingi ya Nadharia ……………………………………..……………17

1.7.1 Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano………………………………………17

1.7.2 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa………………………………………. 20

1.8 Mbinu za Utafiti………………………………………………………. 22

1.8.1 Mahali pa Utafiti……………………………………………………….23

1.8.2 Sampuli na Usampulishaji……………………..…………………......... 24

1.8.3 Mbinu za Ukusanyaji Data………………………………………..... 26

1.8.3.1 Mahojiano………………………………………………………...... 26

1.8.3.2 Uchunzaji……………………………………………………….........27

1.8.4 Maadili ya Utafiti…………………………………………………....28

1.8.5 Uchanganuzi wa Data…………………………………………...……. 28

1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo………………………………………………. 30

1.9 Hitimisho……………………………………………………………….. 30

**SURA YA PILI: STADI ZA KUANDIKA IMLA**

2.0 Utangulizi………………………………………………………………. 31

2.1 Historia ya Maandishi………………………………………………… 32

2.2 Historia ya Somo la Imla……………………………………………… 33

2.3 Uimarishaji wa Stadi ya Kuandika Kupitia Somo la Imla……………… 34

2.3.1 Tahajia……………………………………………………………………40

2.3.1.1 Udondoshaji wa Sauti…………………………………………………42

2.3.1.2 Uchopekaji wa Sauti…………………………………………………...44

2.3.1.3 Ubadilishaji wa Sauti………………………………………………..45

2.3.1.4 Kutenga Silabi…………………………………………………………………47

2.3.2 Sarufi………………………………………………………………….......49

2.3.3 Hati………………………………………………………………………… 52

2.3.4 Msamiati…………………………………………………………………..53

2.3.5 Sauti ……………………………………………………………………….54

2.4 Uchanganuzi wa Matokeo ya Zoezi la Imla…………………………… 54

2.6 Hitimisho…………………………………………………………………….58

**SURA YA TATU: MBINU ZA KUFUNDISHA SOMO LA IMLA NA CHANGAMOTO ZINAZOKABILI WALIMU**

3.0 Utangulizi…………………………………………………………………… 60

3.1. Viwango vya Elimu vya Walimu……………………………………… 61

3.2 Ufundishaji wa Stadi ya Stadi ya Kuandika…………………………… 63

3.3 Ufundishaji wa somo la Imla……………………………………… 65

3.4 Changamoto Zinazowakabili Walimu katika Ufundishaji wa Imla…… 76

3.5 Hitimisho………………………………………………………… 80

**SURA YA NNE: UDHAIFU KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA IMLA**

4.0 Utangulizi………………………………………………………… 81

4.1 Udhaifu Uliojitokeza katika Ufundishaji wa Somo la Imla………… 82

4.1.1 Mbinu za Kufundisha……………………………………………….. 85

4.1.2 Mazingira ya Darasani………………………………………………. 85

4.1.3 Matamshi ya Walimu…………………………………………………. 86

4.1.4 Vitabu na Vifaa vya Kufundishia…………………………………… 87

4.1.5 Maandalizi ya Walimu……………………………………………… 88

4.1.6 Kutosahihisha Kazi za Wanafunzi…………………………………… 89

4.1.7 Uteuzi wa Matini…………………………………………………… 90

4.2 Udhaifu Uliojitokeza katika Ujifunzaji wa Imla………………………… 94

4.2.1 Matamshi na Maandishi ya Wanafunzi………………………………… 94

4.2.2 Kutokuwa Makini katika Somo la Imla………………………………. 95

4.3 Maelekezo ya Silabasi na Vifaa vya Kufundishia……………………… 96

4.4 Hitimisho………………………………………………………………… 98

**SURA YA TANO: MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO**

5.0 Utangulizi……………………………………………………………… 99

5.1 Muhtasari wa Tasnifu…………………………………………………... 99

5.2 Matokeo ya Utafiti……………………………………………………. 101

5.3 Changamoto za Utafiti………………………………………………... 104

5.4 Mchango wa Utafiti ………………………………………………….. 104

5.5 Mapendekezo ………………………………………………………. 105

MAREJELEO…………………………………………………………………….. 108

## VIAMBATISHO


| | | |
|---|---|---|
| Kiambatisho A | Kiongozi cha Mahojiano kwa Walimu……………… | 113 |
| Kiambatisho B | Kiongozi cha Uchunzaji……………………………...... | 114 |
| Kiambatisho C | Kifungu cha Imla……………………………………. | 115 |
| Kiambatisho D | Barua ya shule ya kuidhinisha Utafiti ……………… | 116 |
| Kiambatisho E | Kibali cha NACOSTI……………………………….. | 117 |

## ORODHA YA MAJEDWALI NA VIELELEZO


Jedwali 1.1 Idadi ya Shule za Sekondari katika Gatuzi la Trans-Nzoia… 25

Jedwali 2.1 Mazoezi Yanayotumiwa Kuimarisha Stadi ya Kuandika…… 34

Jedwali 2.2 Vipengele vya Stadi za Lugha katika Somo la Imla………… 36

Jedwali 2.3 Idadi ya Wanafunzi Waliochunzwa…………………………. 37

Jedwali 2.4 Maoni ya Wanafunzi Kuhusu walichojifunza ………………. 38

Jedwali 2.5 Makosa ya Udondoshaji wa Sauti……………………………. 43

Jedwali 2.6 Makosa ya Uchopekaji wa Sauti……………………………… 44

Jedwali 2.7 Makosa ya Ubadilishaji wa Sauti……………………………… 46

Jedwali 2.8 Utengaji wa Silabi……………………………………… 48

Jedwali 2.9 Makosa ya Sarufi………………………………………… 50

Jedwali 3.1 Mbinu Zinazotumiwa na Walimu Kufundishia Somo la Imla …. 67

Jedwali 3.2 Usetaji wa Somo la Imla…………………………………… 70

Jedwali 3.3 Vitate Vinavyohusisha Maneno yenye Sauti f, v na t, d…… 72

Jedwali 3.4 Changamoto katika Uwasilishaji wa Somo la imla………… 76

Jedwali 4.1 Udhaifu katika Ufundishaji wa Imla……………………… 83

Jedwali 4.2 Uteuzi wa Matini kutoka Vipengele vya Lugha…………… 91

Jedwali 4.3 Jinsi Silabasi Inavyoelekeza Ufundishaji wa Imla……..…… 97

Kielelezo 3.1 Viwango vya Elimu vya Walimu…………………………………62

Kielelezo 3.2 Maazimio ya Kazi, Shule B…………………………………... 73\

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| K.C.P.E | Kenya Certificate of Primary Education |
| K.C.S.E | Kenya Certificate of Secondary Education |
| K.I.C.D | Kenya Institute of Curicullum Development |
| K.N.E.C | Kenya National Examination Council |
| NACOSTI | National Commission for Science, Technology and Innovation |
| N.U.M | Nadharia ya Uchanganuzi Makosa |
| L1 | Lugha ya kwanza |
| L2 | Lugha ya pili |
| LL | Lugha lengwa |
| T.S.C | Teachers Service Commission |

# SURA YA KWANZA

## UTANGULIZI

### 1.0 Usuli wa Mada

Imla ni somo la kupima uwezo wa mtu au watu kuandika kwa usahihi maneno yaliyosemwa (Wamitila, 2016). Somo la imla ni mojawapo ya masomo yanayofundishwa katika stadi ya kuandika katika lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Ufunzaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili shuleni umeendelea kukumbwa na matatizo mengi licha ya Kiswahili kupewa hadhi ya kuwa lugha rasmi nchini Kenya. Kulingana na Onyango (1990), baadhi ya matatizo hayo huchangiwa na dhana potovu za wanafunzi kuhusu Kiswahili. Hata hivyo, changamoto zinazoikumba lugha ya Kiswahili ni nyingi zaidi. Kwa hivyo, tafiti nyingi zaidi zinastahili kufanyiwa mada zinazofundishwa darasani, hasa mada katika stadi za kuandika na kuzungumza kwa nia ya kubaini mchango wake katika kuhakikisha kuwa, wanafunzi wanaandika na kutamka kwa ufasaha.

Wanyoike (1978) na Mbaabu (1985) wanaafikiana kuwa watu wanaojifunza lugha ya pili hupata shida kutokana na kuathirika na L1. Wanyoike (1978) anapendekeza utafiti wa kina ufanywe na watu walio na umilisi wa lugha ya Kiswahili. Wanyoike anasisitiza kwamba, matokeo ya utafiti yanaweza kutumiwa na wanaoandaa mitaala katika maandalizi yatakayolenga na kuafiki mahitaji ya wanafunzi. Mwalimu anapaswa kutumia mbinu mahsusi za kufundishia

kumwezesha mwanafunzi wa Kiswahili kupata stadi za kuandika na kutamka (K.I.E, 2005). Odeo na Maina (2008) wanasema kuwa, ingawa lugha ya Kiswahili inafunzwa shuleni, ufundishaji wake unakabiliwa na changamoto nyingi. Matokeo ya haya ni kuwa ufundishaji unakuwa duni na wanafunzi wanaofuzu katika viwango mbalimbali hawafamu Kiswahili kwa ufasaha.

Kulingana na Bishop (1985), ubora wa silabasi si uzuri wa yaliyomo tu bali utekelezaji wake. Shiundu na Omulando (1992) wanaeleza kuwa ingawa utekelezaji wa silabasi shuleni hutegemea mambo kama vile fedha, vifaa na wanafunzi miongoni mwa mengine, jambo lililo muhimu zaidi ni walimu. Walimu wanapaswa kuhakikisha kuwa yaliyomo kwenye silabasi yanawafikia wanafunzi bila kubagua ili kuwawezesha kupata stadi za lugha. Mafunzo ya silabasi katika shule za sekondari yamegawanywa katika stadi nne kuu: kusoma, kuandika, kuzungumza na kusikiliza (K.I.E, 2005). Mwanafunzi anapaswa kupata stadi hizi nne ambazo zimetengwa kutegemea umilisi wake wa kimawasiliano kufikia mwisho wa elimu ya shule ya upili.

Kwa mujibu wa Oller (1971), somo la imla linahusisha stadi zote nne za lugha ya Kiswahili licha ya kuratibiwa katika stadi ya kuandika. Oller (1971) anaongezea kuwa, stadi ya kusikiliza inahusishwa wakati sentensi zinasomwa na mwalimu ili wanafunzi waandike. Wanafunzi wanapaswa kuwa makini ili wasikilize sentensi

zinazosomwa na mwalimu. Stadi ya kuandika inaimarika wakati wanafunzi wanaendeleza yale wanayosikiliza kwa ufasaha. Stadi ya kusoma inakuzwa wakati wanafunzi wanasoma kimoyomoyo baada ya kuandika sentensi ili kurekebisha makosa na hata kwa sauti ili kujifunza matamshi sahihi. Isitoshe, stadi ya kuzungumza inahusishwa wakati sentensi ambazo wanafunzi wanapewa zinatumiwa katika vikundi vya kujadili ili kufahamu miundo ya sentensi na maana ya misamiati mbalimbali. Kwa hivyo, somo la imla linapaswa kutiliwa maanani ili wanafunzi waweze kuwasiliana kwa ufasaha katika maandishi na matamshi.

Kwa upande mwingine, Kawoya na Ryanga (2003) wanasema kwamba kuzungumza ni stadi yenye umuhimu kwa sababu mazoezi ya mwanafunzi katika stadi hii ni msingi mzuri katika kufanikiwa kwake katika lugha andishi. Wanaongeza kusema kwamba, mwanafunzi akiwa na mazoea ya kuzungumza ipasavyo, haitakuwa vigumu kwake kuandika kwa njia inayofaa. Aidha, mwanafunzi akizoea kutamka visivyo, inawezekana matamshi hayo kuathiri anavyoandika. Hii ni kwa sababu, watu wana mazoea ya kuandika kama vile wanavyozungumza. Hivyo basi, kuboresha matamshi ya mwanafunzi ni njia mojawapo ya kukuza uandishi wa mwanafunzi huyo.

Silabasi ya Kiswahili (K.I.E, 2005) imeorodhesha malengo ya stadi ya kuandika kama yafuatayo: kuandika hati zinazosomeka na nadhifu, kuendeleza maneno kwa

usahihi katika maandishi, kuandika sentensi zenye miundo sahihi, kuakifisha kwa njia inayofaa na kuandika maandishi yaliyo na mtiririko. Ili malengo haya yaafikiwe, vipengele vyote vya stadi ya kuandika vinapaswa kufundishwa kikamilifu na kwa undani. Imla ni somo la kujaribiwa maendelezo ya maneno kwa kuyaandika baada ya kutamkiwa (TATAKI, 2013). Mwalimu anapaswa kutamka kisha mwanafunzi aendeleze yanayotamkwa kitabuni bila kuongeza au kuondoa lolote. Nganje na Njogu (2008) wanaeleza kuwa, shabaha ya somo la imla kwa mwanafunzi ni: kujenga usikivu, kuendeleza maneno vizuri, kuandika akizingatia uakifishaji na kuandika kwa wepesi. Usikivu wa wanafunzi unajengeka wakati wanafunzi wanasikiliza kwa makini sentensi wanazosomewa na mwalimu, wakishasomewa sentensi hizo wanapaswa kuziendeleza ipasavyo wakizingatia hati nadhifu na uakifishaji sahihi.

Somo la imla linapendekezwa na watafiti wengi kama vile, Safri (2011), Bowen (2000) na Sakri (2015) kuwa lenye athari kubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa L2. Kulingana na watafiti hawa, somo hili linaweza kutumiwa kuboresha vipengele vya stadi ya kuandika kama vile hijai, utungaji wa sentensi sahihi kisarufi na katika ujenzi wa aya. Kwa hivyo, mazoezi ya imla yanaweza kutumika kukuza vipengele mbalimbali vya stadi ya uandishi kama vile sarufi, maendelezo sahihi ya maneno, uakifishaji unaofaa na msamiati ambao utawawezesha wanafunzi kuwasiliana.

Hata hivyo, tafiti za awali zimeonyesha kuwa somo la imla halipewi uzito unaofaa darasani na huenda sababu hii ikachangia kuwapo kwa makosa mengi katika lugha andishi (Roper, 1989; Kamal, 2005 na Mason, 2012). Kwa hivyo inaonekana kuwa, wanafunzi wanapokosa kufundishwa somo la imla kwa upana wanaweza kuwa na udhaifu wa kuandika yale wanayoyasikia. Aidha, Sarki (2015) anasema kuwa, ufundishaji wa imla kwa kutumia mbinu za kisasa unaweza kuimarisha matokeo ya stadi ya uandishi.

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza ufundishaji na ujifunzaji wa imla darasani kama njia ya kugundua na kuonyesha makosa ya wanafunzi katika stadi ya kuandika kwa kuzingatia mhimili wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa kwamba mtu hujifunza lugha kwa kufanya makosa. Makosa hayo yanaporekebishwa mara kwa mara, mwanafunzi atakuwa amejifunza lugha. Aidha, utafiti huu haukuchunguza ikiwa somo la imla linaboresha matokeo ya wanafunzi bali ulichunguza makosa ya wanafunzi kwa lengo la kubaini vipengele vya stadi ya kuandika ambavyo wanafunzi hujifundisha katika somo la imla. Hili litawawezesha walimu kushughulikia sana sehemu za stadi ya kuandika ambazo zinawatatiza wanafunzi wao. Kulingana na utafiti huu, somo la imla halionyeshi tu matatizo katika maendelezo ya maneno, lakini pia ni njia bora ya kubainisha

makosa ya kisarufi na kisemantiki. Sehemu ifuatayo imechunguza na kuchanganua suala lililofanyiwa utafiti ili kuonyesha kilichochochea utafiti huu kufanywa.

**1.1 Suala la Utafiti**

Utafiti huu ulinuia kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla katika shule za upili katika Gatuzi la Trans-Nzoia, nchini Kenya. Tafiti za awali kama vile; Almatul (2019) alichunguza athari ya somo la imla katika kuimarisha stadi ya kusikiliza. Sakri (2015) naye alichunguza athari ya imla katika kuimarisha stadi ya kuandika katika shule za upili. Hivyo basi, kadri nijuavyo, hakuna utafiti wa awali uliofanywa kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika shule za sekondari ilhali somo la imla lina umuhimu mkubwa katika kuimarisha stadi ya kuandika.

Ufundishaji na ujifunzaji wa imla unapaswa kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaendeleza maneno vizuri na kuakifisha kwa njia inayofaa. Hata hivyo, ripoti za kila mwaka za Taasisi ya Mitihani (KNEC) zinaonyesha kuwa baadhi ya wanafunzi wanafanya makosa mengi ya hijai na sarufi katika maandishi mbalimbali. Somo la imla linapaswa kuimarisha tahajia na sarufi ya mwanafunzi (K.I.E, 2005). Makosa haya hutokana na uendelezaji mbaya wa maneno na uakifishaji usiofaa mtawalia. Mtihani wa Kiswahili (K.C.S.E) umegawanywa katika sehemu tatu; insha, matumizi ya lugha na fasihi. Wanafunzi huadhibiwa

katika mtihani wa insha na ule wa matumizi ya lugha kutokana na makosa ya hijai na sarufi.

Utafiti huu umechunguza vipengele vya stadi ya uandishi ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla na kubaini udhaifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo. Hivyo basi, utafiti huu uliazimia kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla katika kiwango cha sekondari ili kupendekeza jinsi ya kuliboresha. Sehemu inayofuata imeonyesha malengo na maswali yaliyoongoza utafiti huu.

**1.2 Malengo ya Utafiti**

Malengo yaliyoongoza utafiti huu ni:

1) Kutathmini vipengele vya stadi ya uandishi ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla.
2) Kuchunguza mbinu ambazo walimu hutumia kufundishia somo la imla.
3) Kueleza changamoto ambazo walimu hukumbana nazo katika ufundishaji wa somo la imla.
4) Kudhihirisha udhaifu unaojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa imla.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

Maswali yaliyoongoza utafiti huu ni:

1) Je, wanafunzi hujifunza vipengele vipi vya stadi ya uandishi katika somo la imla?
2) Je, walimu hutumia mbinu zipi kufundishia somo la imla?
3) Je, ni changamoto zipi zinazokabili walimu katika ufundishaji wa somo la imla?
4) Je, ni udhaifu upi unaojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa imla?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Mtafiti alinuia kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla kwa sababu somo hili lilipaswa kuboresha stadi za lugha kama vile kuandika na kuongea kwa kiasi kikubwa. Kutokana na umuhimu wa stadi ya kuandika hasa uendelezaji bora wa maneno, walimu wanapaswa kuboresha mbinu za kufundishia imla ili wanafunzi wapate umilisi wa kutosha katika stadi hii ya lugha. Walimu wa Kiswahili wa shule za sekondari wanapaswa kutambua na kuwapa wanafunzi wenye matatizo ya kuendeleza maneno mwelekeo. Aidha, ikiwa kuna udhaifu katika ufundishaji wa somo la imla unahitaji kushughulikiwa kwa kuzingatia mapendekezo aliyotoa mtafiti ili kuboresha somo la imla na stadi ya kuandika kwa ujumla.

Utafiti huu ulitathmini ujifunzaji wa imla kwa sababu kulingana na Mutiga (2008) wanafunzi wengi huhitimu shule ya upili bila kupata ujuzi wa kuzungumza na kuandika. Hivyo basi, kulikuwa na haja ya kutafiti zaidi kuhusu hali hii inayowafanya wanafunzi wasiweze kuandika kwa ufasaha licha ya kufundishwa stadi ya uandishi. Somo la imla lilichunguzwa kwa sababu linapaswa kuimarisha stadi ya uandishi kwa kuondoa makosa ya hijai, sarufi na hata kuimarisha hati za wanafunzi lakini halionekani kutekeleza malengo hayo. Kwa hivyo, utafiti wa nyanjani ulitathmini ujifunzaji wa somo la imla ili kubaini ikiwa kuna udhaifu fulani katika ujifunzaji wa somo hilo unaowafanya wanafunzi wasijifunze kile walimu wanakusudia wajifunze.

Hali kadhalika, utafiti huu ulichochewa na madai ya Mutiga (2008) kwamba ni lazima silabasi ya Kiswahili ishughulikie mahitaji maalum ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2 katika mazingira ya wingi-lugha na wala si ya lugha moja. Utafiti huu ulifanywa katika Gatuzi la Trans-Nzoia nchini Kenya. Kulingana na matokeo ya hesabu ya watu ya mwaka 2009, eneo la Trans-Nzoia lina mchanganyiko wa watu wenye lugha za kwanza tofauti kwa hivyo wengi hutumia Kiswahili kama lugha ya pili ili kuwasiliana. Isitoshe, wanafunzi wengi wanajifunza Kiswahili kama L2 katika gatuzi hili. Kwa sababu hii, utafiti huu ulifanywa kwa kuchukulia ufundishaji wa Kiswahili kama ufundishaji wa L2. Shule za upili ziliteuliwa kwani wanafunzi hawa tayari wametangulizwa katika stadi za lugha wakiwa shule za msingi na wanaendelea kuziboresha. Sehemu hii

imeeleza kwa upana sababu zilizotuchochea kuchagua mada ya utafiti. Sehemu ifuatayo imeweka bayana upeo na mipaka ya utafiti huu.

### 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulitathmini ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika shule za sekondari. Somo la imla linapaswa kufundishwa kama mojawapo ya masomo ya stadi ya uandishi katika shule zote nchini Kenya. Hata hivyo, utafiti wetu ulijikita kuchunguza na kutathmini ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika shule za upili pekee katika Gatuzi la Trans-Nzoia. Gatuzi la Trans-Nzoia ni mojawapo ya magatuzi 47 nchini Kenya linalopatikana upande wa magharibi. Gatuzi hili linajumuisha wilaya tano ambazo ni: Trans-Nzoia Magharibi, Trans-Nzoia Mashariki, Kwanza, Kiminini na Endebes. Ripoti ya hesabu ya watu (2009) inaonyesha kuwa, Gatuzi la Trans-Nzoia lina watu 818,757 ambao wanatoka katika jamii tofauti nchini Kenya. Kulingana na Wizara ya Elimu 2018, Gatuzi la Trans-Nzoia lina wanafunzi 229,042 ambao wanasoma katika shule za msingi ama za sekondari.

Trans-Nzoia ni eneo moja nchini Kenya linalowakilisha maeneo mengine yanayopatikana katika mazingira ya wingi lugha. Hivyo, matatizo mengi yanayokumba ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika Gatuzi la Trans-Nzoia huenda ni yale yale yanayowakumba walimu na wanafunzi kwingineko nchini Kenya. Hususan mtafiti alichunguza walimu na wanafunzi wa kidato cha pili.

Kidato hiki kilichaguliwa kwa sababu wanafunzi walikuwa tayari wamejengewa msingi wa stadi za lugha katika kidato cha kwanza na wanaendelea kuziboresha. Aidha, kulingana na silabasi ya Kiswahili (K.I.E, 2005), stadi zote za lugha zinapaswa kusisitizwa katika kidato cha pili ili kuandaa wanafunzi katika ujifunzaji wa kina na mpana wanaposonga katika madarasa ya juu (kidato cha tatu na cha nne). Sehemu hii imeweka wazi upeo na mipaka ya utafiti huu. Sehemu inayofuata imechunguza maandishi ya kijumla na mahsusi kuhusu ufundishaji na ujifuzaji wa imla.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Sehemu hii imezingatia maandishi ya kijumla kuhusu ujifunzaji na ufundishaji wa L2, ufundishaji wa stadi za lugha kwa ujumla na ufundishaji wa imla kama somo. Aidha, tafiti mbalimbali na malengo ya tafiti hizo, nadharia zilizotumika katika tafiti hizo na matokeo ya tafiti hizo yalishughulikiwa.

Musau (1993) alitafiti kuhusu ujifunzaji na ufunzaji wa L2, kipengele cha fonolojia. Alishirikisha wanafunzi waliokuwa wanajifunza lugha ya pili (Kiswahili). Wanafunzi hao walitoka katika jamii saba ambazo hutumia lugha tofauti: Kikalenjini, Kikamba, Kibukusu, Kisomali, Kikuyu, Kimasai na Kiluo. Utafiti wake ulizingatia matamshi yaani namna ya kutamka na kuelewa fonolojia ya Kiswahili. Lengo lake kuu lilikuwa kubainisha masuala yanayochangia muundo

wa fonolojia ya mwanafunzi wa Kiswahili. Ilibainika kuwa mwanafunzi anapojifunza L2, anaweza kuhamisha baadhi ya sauti kutoka L1. Ugumu hutokea anapokumbana na sauti ngeni katika L2. Musau anapendekeza kutiliwa maanani kwa jambo hili na wakuza mitaala wanapoandaa mitaala na vifaa vya kufundishia pamoja na ufunzaji wenyewe. Kazi hiyo inaingiliana na utafiti huu kwa sababu zote zinashughulikia ujifunzaji wa Kiswahili kama L2.

Ngugi (2008) alifanya utafiti kuhusu mtaala wa Isimujamii katika shule za upili. Madhumuni yake yalikuwa kuchunguza jinsi walimu wanavyotekeleza mtaala wa Isimujamii na changamoto zinazokumba utekelezaji wa mtaala huo kwa shule za upili. Alitumia nadharia ya lugha ya mawasiliano kutathmini mbinu zilizotumiwa na walimu kufundishia somo la Isimujamii na changamoto zinazowakumba walimu katika utekelezaji wa mtaala wa Isimujamii. Katika matokeo yake, alibaini kuwa miundo ya lugha inasisitizwa na walimu wengi badala ya uamilifu wa lugha. Utafiti wake pia ulionyesha kuwa ukosefu wa vifaa vya kufundishia unatinga utekelezaji wa mtaala wa Isimujamii. Utafiti wake ni tofauti na wetu kwani alitathmini mtaala wa Isimujamii na wetu umetathmini ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika shule za upili.

Okoba (2008) alichunguza jinsi wanafunzi walivyojifunza kusoma kwa sauti katika shule za msingi hususan madarasa ya chini. Utafiti wake ulichunguza

nyenzo na mbinu ambazo walimu walitumia walipofundisha stadi ya kusoma. Matatizo yaliyowakabili watoto katika usomaji pia yalichanganuliwa. Alitumia nadharia ya Krashen pamoja na Modeli Husishi. Utafiti wake ulifanywa katika wilaya ya Thika. Matokeo yalidhihirisha kuwa, wanafunzi hawakuwa na msingi dhabiti katika stadi ya kusoma kwa sauti na hili liliathiri kuimarika kwao katika stadi ya kusoma katika madarasa ya juu. Utafiti wake unakaribiana na huu kwani tafiti zote zinahusu mbinu za ufundishaji wa stadi za lugha na udhaifu unaojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi hizo. Utafiti wake ni tofauti na huu kwani alichunguza stadi ya kusoma na utafiti huu umechunguza stadi ya kuandika katika lugha ya Kiswahili.

Karingi (2012) alichunguza jinsi wanafunzi walivyojifunza vivumishi na vibainishi katika shule za sekondari. Malengo yake yalikuwa kubainisha mbinu za ufunzaji wa vivumishi na vibainishi, kuchanganua matatizo wanayopata wanafunzi na walimu katika kujifunza na kufunza vivumishi na vibainishi na kutathmini chanzo cha matatizo hayo. Alitumia nadharia ya sintaksia finyizi kutathmini chanzo cha matatizo na athari ya makosa ya kisintaksia katika kufunza na kujifunza vivumishi na vibainishi. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa, matatizo makuu yanayowakumba wanafunzi katika kujifunza kategoria hizi za maneno yanatokana na mbinu za kufunza. Utafiti wake unakaribiana na huu kwani tafiti zote zinahusu mbinu za kujifunza na kufundisha Kiswahili katika shule za upili.

Utafiti wake unatofautiana na huu kwani alichunguza jinsi ya kufundisha na kujifunza vibainishi na vivumishi na wetu ulichunguza ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika shule za sekondari. Aidha, alifanya utafiti wake wilayani Kirinyaga ambako asilimia kubwa ya wanafunzi waliathiriwa na L1 ya Kikuyu na utafiti huu ulifanywa katika Gatuzi la Trans-Nzoia ambapo, kulingana na Gakuo (2014), ni eneo lenye mchanganyiko wa lugha zote nchini Kenya.

Odeo na wenzake (2008) walichunguza jinsi walimu walivyotumia maswali zungumzi, idadi ya maswali hayo, aina na ufaafu wa maswali hayo kimaana na kimuundo. Utafiti huo pia ulichunguza majibu ya wanafunzi kwa njia ya mdomo ukizingatia idadi, aina na ufaafu wa majibu hayo kama ilivyobainika katika urefu, maana na muundo. Utafiti huo uliongozwa na nadharia ya Krashen na ulifanywa katika Gatuzi la Bungoma, magharibi mwa nchi ya Kenya. Data ilikusanywa kutumia mbinu ya uchunzaji, kurekodi sauti na mahojiano ya moja kwa moja na walimu. Matokeo yalionyesha kwamba, kulingana na ufaafu wa maswali, thuluthi mbili yalikuwa changamano na yalihusiana na sarufi. Hata hivyo, maswali mengi yalikuwa ya kiwango cha chini. Aidha, utafiti huo ulionyesha kuwa mazingira ya darasani yalitinga utoaji wa majibu. Utafiti huo unakaribiana na wetu kwani unahusu kuuliza maswali kwa njia ya mdomo na somo la imla linahusu mwalimu kutamka na wanafunzi kuandika. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwani ulijikita

katika kuuliza maswali pekee na wetu ulihusu jinsi wanafunzi wanavyobadilisha lugha zungumzi hadi andishi ili kuimarisha stadi ya uandishi.

Fisher (2001) alitafiti jinsi wanafunzi wanavyojifunza somo la imla na kile wanachojifunza kutoka somo hilo. Alitumia nadharia ya fonimu ya Ferdinand de Saussure kutathmini jinsi wanafunzi katika vyuo vya Japani walivyojifunza imla katika lugha ya Kiingereza. Wanafunzi hao walikuwa wamefunzwa Kiingereza kutoka shule ya msingi hadi sekondari licha ya kutumia Kijapani kama lugha yao ya kwanza. Fisher alitaka kujua ni nini wanafunzi hujifunza katika somo la imla. Matokeo ya utafiti wake yalikuwa kwamba, somo la imla lina manufaa mengi kama vile linaimarisha stadi za lugha za mwanafunzi na linampa mwalimu habari muhimu kuhusu ufahamu wa lugha wa mwanafunzi. Utafiti wake unafanana na huu kwani tafiti zote zinahusu somo la imla kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Utafiti wake unatofautiana na huu kwani alichunguza wanafunzi katika vyuo vikuu nasi tulichunguza wanafunzi katika shule za sekondari.

Sarki (2015) alifanya utafiti kuhusu jinsi somo la imla linavyoathiri ufundishaji wa lugha andishi ya Kiingereza katika shule za upili za Nigeria. Alilenga kuchunguza jinsi somo la imla linavyaimarisha lugha andishi ya Kiingereza katika vidato vya chini katika shule za upili. Alitumia vigeu kama vile maendelezo ya maneno, ujenzi wa sentensi na aya kutekeleza utafiti wake. Aliwapa wanafunzi mada za

insha ili waandike kisha akateua asilimia 10 ya kazi hizo kwa kutumia sampuli kusudi na kuzichanganua. Matokeo yalionyesha kuwa, ufundishaji wa imla ulikuwa na athari kubwa ambayo ni chanya katika ujenzi wa sentensi na aya katika lugha andishi ya Kiingereza. Aidha, utafiti wake uligundua kuwa hakukuwa na athari kubwa ya ufundishaji wa imla katika maendelezo ya maneno. Hivyo basi, utafiti huu ulipendekeza kuwa, somo la imla linaweza kutumiwa kuimarisha vipengele kadha vya lugha andishi kama vile ujenzi wa sentensi na aya. Utafiti wake unakaribiana na huu kwa sababu tafiti zote zinahusu somo la imla katika shule za upili. Hata hivyo, utafiti wake ni tofauti na huu kwa sababu ulichunguza jinsi somo la imla linavyoimarisha lugha andishi ya Kiingereza nchini Nigeria lakini huu umechunguza ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla katika shule za upili nchini Kenya.

Alimatul (2019) alichunguza athari ya matumizi ya mbinu ya imla katika kuimarisha stadi ya kusikiliza ya wanafunzi wa gredi ya 11. Matokeo yalionyesha kuwa, somo la imla lina athari chanya katika kuimarisha stadi ya kusikiliza ya wanafunzi. Utafiti wake unalingana na huu kwa sababu zote zinazungumzia ufundishaji wa somo la imla. Aidha, utafiti wake unatofautiana na huu kwa sababu ulichunguza jinsi somo la imla imla linavyoimarisha stadi ya kusikiliza lakini utafiti huu umechunguza jinsi somo la imla linavyofundishwa na vipengele vya stadi ya kuandika ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla.

Baada ya kuchunguza maandishi ya kijumla kuhusu stadi ya uandishi na kuelezea maandishi mahsusi kuhusu somo la imla, Sehemu ifuatayo imejadili misingi ya nadharia iliyoongoza utafiti huu.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa zilituongoza katika utafiti huu. Nadharia ya lugha ya mawasiliano ilitumiwa kuonyesha na kuchanganua mbinu ambazo walimu hutumia kufundishia somo la imla na changamoto zinazowakabili wakifundisha somo hilo. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ilitumiwa kuonyesha vipengele vya lugha ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla na udhaifu unaojitokeza katika ujifunzaji wa somo la imla ili kupendekeza mbinu za kuliboresha. Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, watu hujifunza L2 vyema kwa kufanya makosa ambayo yanastahili kutambuliwa na kurekebishwa. Sehemu ifuatayo imechunguza kwa kina Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano na kuonyesha jinsi ilivyotuelekeza katika utafiti huu.

### 1.7.1 Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano

Nadharia hii iliasisiwa katika miaka ya 1960 nchini Uingereza kabla ya kuenea kote ulimwenguni (Richards na Rodgers, 1986). Kuanzia mwaka wa 1960

kuendelea, kulikuwa na imani kuwa ujuzi wa miundo au vipengele vya lugha ulimtambulisha mwanalugha. Kama McDonough na Shaw (1993) wanavyosema, mwanafunzi wa lugha alistahili kujua miundo ya lugha pekee. Wanaendelea kusema kwamba, ingawa umilisi wa miundo ni muhimu, hautoshi kwa sababu baadhi ya wanafunzi wenye umilisi wa miundo wanaweza kuunda sentensi sanifu, lakini wasiweze kuzitumia kwenye mawasiliano yao ya kila siku.

Miaka ya 1970, muundo wa maumbo ya lugha ulianza kukashifiwa na wanaisimu. Walisisitiza kwamba, wanafunzi wanapaswa kuwa na umilisi wa mawasiliano licha ya kuwa na umilisi wa lugha. Waasisi wa mtazamo huu kama Hymes (1971) na Halliday (1964) wanaonelea kuwa anayejifunza lugha lazima awe na uwezo wa kuitumia vilivyo. Huu ndio uamilifu wa mawasiliano kwa vile humpa uwezo anayejifunza L2 kuitumia katika miktadha mbalimbali. Kwa hivyo ufundishaji wa lugha ukachukua mtazamo mwingine na msisitizo ukawa wanafunzi lazima wawe na uamilifu wa mawasiliano licha ya kuwa na umilisi wa lugha. Utafiti huu ulichunguza ikiwa wanafunzi wanaweza kuendeleza maneno kwa ufasaha baada ya kufundishwa stadi ya imla.

Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano inapendekeza hatua kadhaa kuchukuliwa ili ujifunzaji na ufundishaji huo utimilike. Kwa mujibu wa Johnson (1982), ufundishaji wa lugha ya mawasiiliano utaimarika ikiwa kutakuwa na mazoezi mengi ya lugha inayofunzwa. Ni kupitia matumizi ya lugha hiyo ambapo

wanafunzi wanaweza kuwasiliana (Rivers, 1983). Lugha itakuwa na maana na kuonekana yenye manufaa kwa wanafunzi na kwa hivyo kuwapa motisha ya kuendelea kujifunza. Shughuli hizi zote hufanya ufundishaji wa L2 rahisi na kuwa na athari kubwa kwa wanafunzi. Jambo hili linaungwa mkono na Willis na Willis (1996) ambao wanasema kuwa, kupitia shughuli hizi, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kuwasiliana kwa lugha hiyo na matumizi yatadumu. Wazo hili pia linashadidiwa na Musau na Chacha (2001) ambao wanasema kuwa Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano inatazamiwa kukuza mbinu za kufundisha zinazosisitiza jinsi miundo ya lugha na mawasiliano inavyohusiana.

Utafiti huu uliongozwa na misingi ya Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano ifuatayo kwa mujibu wa Richards na Rodgers (1986):

i. Lugha inapaswa kutumiwa mara nyingi darasani ili mwanafunzi aweze kujifunza lugha hiyo. Mhimili huu ulimfaa mtafiti alipowahoji walimu ili kujua wanafunza stadi za kuandika mara ngapi kwa muhula. Imla ni mojawapo ya stadi za kuandika na mtafiti amechunguza ikiwa kuna udhaifu wowote katika matumizi ya mazoezi ya imla kuimarisha stadi ya kuandika.
ii. Katika ufundishaji, muktadha wa mawasiliano hupewa umuhimu. Mwalimu alipoteua makala ya kuwasomea wanafunzi, alichopeka msamiati na maneno yaliyo na miundo tofauti katika sentensi. Baada ya somo la imla, mtafiti alifanya mahojiano yasiyo rasmi na wanafunzi ili kutambua

ikiwa somo la imla limewasaidia kujifunza mambo mengine kando na kuendeleza maneno kwa ufasaha.

iii. Mada za kufundishwa huandaliwa kwa kuzingatia mahitaji ya wanafunzi. Utafiti huu ulifanywa katika shule za sekondari zilizo na wanafunzi tofauti walio na viwango mbalimbali. Kwa mfano, mtafiti aliteua shule ya kitaifa, shule ya kaunti na shule ya wilaya, shule hizi zina wanafunzi walio na viwango mbalimbali. Kabla ya mwalimu kuteua makala yaliyotumika kufundishia somo la imla, alizingatia uwezo tofauti wa wanafunzi wake. Aidha, mbinu za ufundishaji wa somo la imla zitakuwa tofauti kulingana na uwezo wa wanafunzi katika shule tofauti.

Kwa kuwa Nadharia ya Lugha ya mawasiliano haikuwa na vigezo vya kuchunguza makosa katika ujifunzaji wa lugha, mtafiti aliamua kutumia nadharia ya pili ambayo ingefanikisha sehemu hii ya utafiti. Nadharia hii ambayo ni ya Uchanganuzi makosa imeshughulikiwa katika sehemu ifuatayo.

### 1.7.2 Nadharia ya Uchanganuzi Makosa

Nadharia ya uchanganuzi makosa iliasisiwa na Corder (1967). Kwa mujibu wa nadharia hii, kuna vyanzo vingi vya makosa mbali na athari ya L1. Nadharia hii inatoa mchango katika kubaini mikakati ambayo wanafunzi hutumia wanapojifunza L2 na kutambua vyanzo vya makosa ya wanafunzi hao.

Kwa upande mwingine, Norrish (1983), anatazama makosa ya wanafunzi kama jambo la kawaida. Anasema kwamba, makosa yanaonyesha kuwa kuna maendeleo katika kujifunza lugha fulani. Aidha, anaongeza kuwa, kuna faida kwa wanafunzi wafanyapo makosa kwa sababu wanakosolewa na kupewa maelekezo yanayofaa na walimu wao.

Corder (1967) anasema kwamba, makosa ya mwanafunzi yanaweza kuwa na umuhimu mkubwa kwa mwalimu. Kwanza, mwalimu anaweza kutambua ikiwa mbinu anazotumia kufundisha zinafaa au la. Isitoshe, mwalimu anaweza kufahamu yote ambayo mwanafunzi wake amejifunza na kile ambacho hajatambua katika L2. Mbali na hayo, mwalimu huweza kubaini iwapo ameafikia malengo yake ya kufundisha. Mwisho, mwalimu hupata kutambua vipengele vinavyohitaji kupewa umuhimu katika ufunzaji wa Kiswahili kwa jumla.

Kulingana na Elis (1997), makosa hutokea kwa kutofuata sheria za lugha. Anaongeza kuwa, iwapo kosa linaweza kukosolewa na mwanafunzi mwenyewe, basi ni jepesi na halipaswi kushughulikiwa. Ikiwa mwanafunzi hawezi kujikosoa mwenyewe, inaonyesha kuwa hana umilisi wa lugha na tatizo hilo linapaswa kushughulikiwa ipasavyo. Makosa yanaweza kuwa wazi au yasidhihirike katika maandishi (Corder, 1973). Aghalabu, makosa yaliyo wazi hutambulika kwa urahisi kati sentensi kama vile yale ya sarufi. Makosa yasiyokuwa wazi kwa upande mwingine huchukuliwa kuwa sahihi kisarufi lakini kisemantiki sentensi hizo

hazina maana. Utafiti huu ulichunguza makosa yaliyo wazi katika uandishi wa imla ili kuyabainisha na kuonyesha athari yake kwa wanafunzi wa Kiswahili.

Kwa mujibu wa Corder (1967), mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ni kama ifuatayo:

i) Mwanafunzi anaweza kufanya makosa anapojifunza L2. Kwa mfano, makosa wanayofanya wanafunzi wanapojifunza zoezi la imla.

ii) Ni kawaida kwa mwanafunzi kufanya makosa anapojifunza lugha na hapaswi kuadhibiwa ila makosa hayo yatumike kuonyesha kuwa mwanafunzi hana umilisi wa lugha. Kwa hivyo, hatua zifuatazo zitekelezwe:

-Kutambua makosa ya mwanafunzi. Mtafiti alihudhuria somo la imla na kutambua makosa yaliyojitokeza katika somo hilo.

-Kuainisha makosa ya mwanafunzi. Baada ya kuhudhuria somo la imla mtafiti aliainisha makosa kama vile hijai na sarufi ili kutambua vipengele vya lugha andishi ambavyo mwanafunzi hujifundisha katika somo la imla.

-Kupendekeza njia bora ya kurekebisha makosa. Mtafiti alipendekeza njia bora za kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla ili kuondoa udhaifu uliojitokeza katika uwasilishaji na upokezi wa somo hilo.

## 1.8 Mbinu za Utafiti

Orodho (2003) anaeleza mbinu za utafiti kuwa mwongozo au utaratibu unaotumiwa kuzua majibu kwa maswali ya utafiti. Sehemu hii imeshughulikia:

mahali pa kufanyia utafiti, sampuli na usampulishaji, maadili ya utafiti; mbinu za kukusanya na kuchanganua data na jinsi ya kuwasilisha matokeo.

**Muundo wa Utafiti**

Utafiti huu ulitumia muundo wa maelezo ya kisoroveya. Usoroveya hujihusisha na kueleza, kurekodi, kutathmini na kuwasilisha hali ambayo ipo au ilikuwepo. Muundo huu ni muhimu kukusanya data nyingi kwa muda mfupi. Lengo kuu la muundo wa kisoroveya ni kukusanya data fulani ili kueleza hali zilizopo (Mugenda na Mugenda, 2019). Hivyo basi, muundo huu ulimsaidia mtafiti kukusanya data kuhusu somo la imla ili kuitathmini, kuichanganua na baadaye kuiwasilisha. Sehemu ifuatayo imeonyesha mahali ambapo utafiti huu ulifanywa.

### 1.8.1 Mahali pa Utafiti

Data za utafiti zilikusanywa nyanjani. Mtafiti aliteua shule tano katika Gatuzi la Trans-Nzoia ambazo alichunguza na kukusanya data. Aidha, mtafiti alipitia vitabu vya kiada na kuchunguza silabasi ili kupata data zaidi kuhusu ufundishaji wa somo la imla.

Utafiti huu ulifanywa katika Gatuzi la Trans-Nzoia ambalo ni eneo moja linalowakilisha sehemu nyingine nchini Kenya zinazopatikana katika mazingira ya wingi lugha. Wanafunzi wengi wanajifunza Kiswahili kama L2 katika gatuzi hili. Aidha, utekelezaji wa mtaala hutegemea kwa kiasi kikubwa hali katika ngazi za

shule hasa yanapohusika masuala ya maandalizi ya walimu, mazingira, vifaa, mitazamo na vitabu (Hawes, 1979; Benaars, Otiende na Boisvert, 1994). Mtafiti alitumia njia ya mahojiano na uchunzaji kupata data kutoka kwa walimu kuhusu mbinu walizotumia kufundisha somo la imla na changamoto zinazowakumba wanapofundisha somo hilo.

### 1.8.2 Sampuli na Usampulishaji

Utafiti huu ulitumia sampuli kusudi kuteua eneo la utafiti. Hii ni kwa sababu sampuli kusudi hulenga makundi maalum katika jamii na makundi hayo huchukuliwa kuwa yanawakilisha makundi mengine halisi (Kombo na Tromp, 2006). Licha ya kuwa kuna sehemu nyingine nchini Kenya ambazo watu hutumia Kiswahili kuwasiliana, Gatuzi la Trans-Nzoia liliteuliwa kimakusudi kulingana na maoni ya Gakuo (2014) kwamba eneo la Trans-Nzoia lina mwingiliano wa watu wa jamii tofauti nchini Kenya ambao hutegemea Kiswahili kuwasiliana. Mbinu tabakishi ilitumika kuteua shule zilizohusishwa katika utafiti huu. Kwa kutumia mbinu tabakishi, shule ziligawanywa katika vikundi mbalimbali kama vile; za kitaifa, mkoa, wilaya au kibinafsi.

**Jedwali 1.1: Idadi ya Shule za Upili katika kaunti ya Trans-Nzoia 2018**

| GATUZI NDOGO | IDADI YA SHULE | | JUMLA |
|---|---|---|---|
| | **SERIKALI** | **KIBINAFSI** | |
| T/NZOIA WEST | 42 | 7 | 49 |
| T/NZOIA EAST | 73 | 2 | 75 |
| KIMININI | 62 | 5 | 67 |
| KWANZA | 46 | 6 | 52 |
| ENDEBES | 18 | 0 | 18 |
| JUMLA | 241 | 20 | 261 |

Gatuzi la Trans-Nzoia lina shule mia mbili sitini na moja. Shule katika gatuzi hili zimegawanywa katika magatuzi madogo matano ambayo ni; Trans-Nzoia Magharibi, Trans-Nzoia Mashariki, Kiminini, Kwanza na Endebes. Gatuzi ndogo la Trans-Nzoia Magharibi liliteuliwa kwani lina viwango vyote vya shule zinazowakilisha shule zote zilizoko nchini Kenya na wanfunzi wengi wanatoka katika maeneo ya wingi lugha. Mtafiti alifikia uamuzi huo kutokana na madai ya Mutiga (2008) kwamba ni lazima silabasi ya Kiswahili ishughulikie mahitaji maalum ya wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kama L2 katika mazingira ya wingi-lugha na wala si ya lugha moja. Eneo la Trans-Nzoia Magharibi lina shule arubaini na tisa (49) lakini mtafiti aliteua shule tano pekee ambayo ni asilimia kumi ya jumla ya shule zote katika eneo hili.

Baada ya kuweka shule katika makundi, mbinu bahatishi ilitumika kuteua shule moja katika kila kundi. Shule zilizoteuliwa ni shule ya upili ya St. Brigids, St. Anthony, Greenfields, Milimani na Shule ya Wasichana ya Tuwan. Msingi wa uteuzi huu ni kuwa shule tano zimetosha kuchunguza jinsi somo la imla linavyowasilishwa na kupokelewa katika shule za upili kama Milroy (1987) anavyosema kuwa sampuli ndogo ya utafiti wa isimu imetosha kwa vile sampuli kubwa huweza kukanganya mtafiti anapoichanganua. Aidha, utafiti awali ulionyesha kuwa somo la imla linafundishwa katika shule zilizoteuliwa.

### 1.8.3 Mbinu za Ukusanyaji Data

Mtafiti alitumia mbinu za mahojiano na uchunzaji ili kukusanya data yake. Mbinu hizi zilitumika nyanjani ili mtafiti aweze kupata data aliyoweza kuchanganua ili kufanikisha utafiti wake. Mbinu hizo za mahojiano na uchunzaji zimejadiliwa katika semu ifuatayo.

#### 1.8.3.1 Mahojiano

Kuhoji ni kukusanya data kwa kuwauliza walengwa maswali na kupata majibu kutoka kwao (Mugenda na Mugenda, 2019). Kuna aina nyingi za mahojiano kama vile mahojiano ya simu na ya moja kwa moja. Mtafiti aliwahoji walimu moja kwa moja na kupata maoni yao kuhusu mbinu walizotumia kufundisha somo la imla na changamoto walizokumbana nazo walipofundisha somo hilo. Aidha, mtafiti alitumia mahojiano yasiyo rasmi kuwahoji wanafunzi ili kuthibitisha maoni ya

walimu. Misingi ya Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano ilitumika kuchunguza mbinu za ufundishaji wa somo la imla na changamoto zilizowakumba walimu walipofundisha somo hili. Mahojiano yaliendeshwa ana kwa ana kwa kutumia kiongozi cha maswali mahususi. Mtafiti alitumia kalamu na karatasi kuandika hoja muhimu wakati wa mahojiano. Aidha, kinasa sauti kilitumiwa ili kunasa hoja ambazo mtafiti huenda aliziwacha nje wakati alipokuwa akiandika. Mtafiti alitumia mahojiano kwa sababu, kulingana na Seliger na Shohamy (1989), mbinu hii humwezesha mtafiti kufafanua vipengele tata vya maswali na kudadisi zaidi ambapo majibu hayakukamilika.

### 1.8.3.2 Uchunzaji

Mtafiti alitumia mbinu hii kukusanya data kutoka kwa wanafunzi na walimu. Kabla ya kuhudhuria darasa lililofundishwa somo la imla, mtafiti aliteua makala aliyompa mwalimu awasomee wanafunzi. Katika somo hilo, mtafiti alitazama jinsi mwalimu alivyofundisha somo hilo na jinsi wanafunzi walivyonakili waliyosomewa na mwalimu. Aidha, mtafiti alichunguza ikiwa kuna udhaifu wowote katika mbinu za uwasilishaji unaoweza kusababisha wanafunzi kunakili kisichokusudiwa. Baada ya somo, mtafiti aliteua madaftari machache akitumia mbinu bahatishi ili aweze kutazama jinsi wanafunzi walivyoendeleza makala waliyosomewa na mwalimu. Sehemu ifuatayo imeonyesha maadili yaliyozingatiwa katika utafiti huu.

### 1.8.4 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alipata kibali cha Shule ya Shahada za Juu na Idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta kabla ya kuruhusiwa kwenda nyanjani. Kwa kuwa utafiti ulihusisha shule mbalimbali katika Gatuzi la Trans-Nzoia, mtafiti aliandika barua kwa walimu wakuu wa shule hizo ili kuwaomba ruhusa ya kufanya utafiti katika shule zao. Aidha, mtafiti aliomba ruhusa kutoka kwa Mkuu wa Elimu wa Gatuzi la Trans-Nzioa ili akubaliwe kufanya utafiti katika gatuzi hilo. Walimu waliohusika katika utafiti huu pia waliombwa ruhusa na kufahamishwa kuwa maoni yao yalitumika katika utafiti huu pekee. Ili kuweza kutangamana na wanafunzi na kupata data kutoka kwao, mtafiti alipata idhini kutoka kwa mwalimu mkuu wa shule husika kwani kufikia wazazi wote ilikuwa vigumu kwa sababu ya muda. Aidha, mtafiti aliomba kibali kutoka katika shirika la utafiti la NACOSTI ili aruhusiwe kufanya utafiti wake nyanjani. Sehemu inayofuata imeonyesha jinsi mtafiti alivyachanganua data alizokusanya katika utafiti huu.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu umechanganua ufundishaji na ujifunzaji imla katika shule za sekondari. Matini ya uchanganuzi ilipatikana kwa kuzingatia maoni ya walimu wakati wa mahojiano. Idadi ya mbinu walizotumia walimu kufundisha somo la imla iliwasilishwa katika majedwali. Baada ya kuwahoji walimu, mtafiti aliainisha mbinu tofauti zilizotajwa na walimu zilizotumiwa kufundishia somo la imla. Aliainisha mbinu hizo za uwasilishaji akitumia misingi ya Nadharia ya Lugha ya

Mawasiliano. Kulingana na Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano, mbinu zinazotumiwa katika kufundisha lugha sharti zizingatie mahitaji ya wanafunzi. Mtafiti alichunguza mbinu walizotumia walimu kufundishia na kuona ikiwa zinakidhi mahitaji ya wanafunzi wa viwango mbalimbali.

Maoni ya walimu yamekadiriwa kupitia asilimia ifuatavyo:

$X/Y \times 100 = \%$ ambapo X = Idadi ya walimu waliotoa maoni yao

Y= Idadi ya walimu walioshiriki katika utafiti

Aidha, data nyingine ilipatikana kwa kuhudhuria somo la imla na kutazama jinsi lilivyoendelezwa. Data iliyotokana na uchunguzi wa darasani ilichanganuliwa ili kuthibitisha majibu kutoka kwa walimu kwenye mahojiano. Aghalabu, matokeo ya uchanganuzi yametolewa kwa njia ya maelezo. Kadhalika, uchanganuzi ulihusu kategoria mbalimbali za makosa waliyofanya wanafunzi walipojifunza imla. Mtafiti aliorodhesha makosa kama vile ya sarufi na hijai baada ya kuhudhuria somo la imla ili kubaini vipengele vya lugha walivyojifunza wanafunzi katika somo la imla kwani kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, watu hujifunza lugha vyema kwa kufanya makosa. Sehemu inayofuata imeonyesha jinsi matokeo ya utafiti huu yalivyochanganuliwa.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Uwasilishaji wa matokeo umetekelezwa kupitia maandishi, majedwali na grafu. Matokeo yaliyotokana na mahojiano rasmi na yasiyo rasmi yaliwasilishwa kwa maandishi. Kutokana na mazungumzo hayo, maoni mbalimbali yaliyotolewa yalinukuliwa na kuandikwa. Matokeo ya uchunzaji yaliwasilishwa katika majedwali na grafu. Majedwali yalitumika kudhihirisha aina ya makosa waliyofanya wanafunzi ili kubaini walichojifunza katika somo la imla. Sehemu inayofuata ndiyo inayotamatisha sura ya kwanza kwa kueleza kwa kifupi yaliyoshughulikiwa katika sura hii.

## 1.9 Hitimisho

Sura hii imechunguza vipengele vya kimsingi katika utafiti huu kama vile; usuli wa mada, suala, malengo na maswali ya utafiti, sababu za kuchagua mada ya utafiti, upeo na mipaka ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Aidha, sura hii ina malengo ambayo yalipaswa kutimizwa kufikia mwishoni mwa utafiti huu. Sura inayofuata imechunguza vipengele vya stadi ya uandishi ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla kwa kutumia Nadharia ya Uchanganuzi Makosa.

# SURA YA PILI

# STADI YA KUANDIKA IMLA

## 2.0 Utangulizi

Lengo la sura hii ni kubainisha vipengele vya stadi ya kuandika ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla. Ufahamu wa vipengele vya stadi ya kuandika katika somo la imla ni muhimu katika utafiti huu. Vipengele hivi vimesaidia kuweka msingi wa sura zilizofuata baadaye. Sura hii imefafanua vipengele mbalimbali vya stadi ya kuandika katika somo la imla kama vile; tahajia, uakifishaji, hati, msamiati na sarufi katika maandishi. Sehemu hii imeongozwa na msingi wa pili wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1971) inayoeleza kwamba, katika kujifunza lugha, mwanafunzi anaweza kufanya makosa. Anapofanya makosa, hapaswi kuadhibiwa bali ichukuliwe kuwa bado hajajifunza lugha na hatua mwafaka zichukuliwe. Makosa hayo yanapaswa kutambuliwa na kuainishwa.

Ili kufanikisha utafiti huu kuhusu vipengele vya lugha ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla, mtafiti alihudhuria darasa linalofundishwa somo la imla. Kabla ya kuhudhuria somo hilo, mtafiti aliteua kifungu alichompa mwalimu awasomee wanafunzi. Makala hayo yaliteuliwa kutoka katika kitabu cha kiada cha kidato cha pili (KLB, 2018). Mtafiti aliwahoji walimu wa kidato cha pili, kisha akahudhuria somo la imla lililofundishwa na walimu hao na kuchunguza makosa waliyofanya wanafunzi waliochunzwa ili kubaini kile walichopaswa kujifunza

katika somo la imla. Hata hivyo, katika kuweka msingi wa sura hii, ni muhimu kueleza historia fupi ya maandishi pamoja na somo la imla ili kutoa fursa ya kulijadili somo hili. Sehemu ifuatayo imechunguza historia ya maandishi kwa ujumla.

## 2.1 Historia ya Maandishi

Imla ni mojawapo ya masomo yanayofunzwa katika stadi ya kuandika. Kwa kuwa somo la imla linahushisha maandishi, ni vyema kueleza historia fupi ya maandishi. Kulingana na Ndalu na wengine (2014), maandishi ni kazi yenye alama zilizotiwa katika eneo fulani kama vile karatasi au mawe ambazo zinaweza kusomwa na kueleweka. Fischer (2003) anasema kuwa maandishi huwa mfumo wa lugha ambao hutegemea mifumo mingine kama vile usemi, msamiati, sarufi na semantiki pamoja na ishara ambayo huwa katika muundo wa alfabeti rasmi.

Hakuna uhakika wa ni lini na wapi maandishi yalianza duniani. Wanahistoria wanaojihusisha na asili ya maandishi wanadai ya kuwa yalianzia huko Sumeria, Mesopotamia. Kulingana na Powell (2009), watu wa Mesopotamia walitumia maandishi ya alama au picha fulani zilizowakilisha neno au wazo. Wasumeria walivumbua maandishi ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano katika shughuli zao za biashara ya masafa marefu. Biashara iliponoga huko Mesopotamia, basi pakawa na haja ya mawasiliano hasa kwa kutumia maandishi.

Kulingana na maandishi ya Biblia, baada ya lugha simulizi ya wanadamu kuvurugwa huko Babeli, mitindo mbalimbali ya kuandika ilianzishwa. Watu walioishi Mesopotamia kama vile wasumeria na wababiloni walianza kutumia maandishi ya michoro, ambayo walichora kwenye udongo uliokuwa majimaji kwa kutumia kifaa chenye ncha kali. Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa, karatasi zimetumika katika kuhifadhi maandishi. Wanafunzi katika shule za upili hurekodi kazi zao kwenye madaftari baada ya kupokea usemi kutoka kwa walimu wao. Baada ya kuchunguza historia ya maandishi, sehemu inayofuata imechunguza historia ya somo la imla ambalo ni sehemu ya stadi ya uandishi.

## 2.2 Historia ya Somo la Imla

Kulingana na Oller na Streiff (1975), somo la imla lina historia ndefu. Kuiga na kukariri ndizo mbinu zilizotumiwa kujifunza mambo mengi katika L1 kabla ya karne ya 16. Katikati ya karne ya 16, mazoezi ya imla yalitumiwa kupitisha yaliyomo kwenye kozi kutoka kwa mwalimu hadi kwa mwanafunzi. Mwishoni mwa karne ya 16, somo la imla lilitumiwa kujifunza lugha za kigeni. Katika karne ya 19, somo la imla lilitumiwa kwa upana pamoja na mbinu ya tafsiri ya lugha kufundishia lugha za kigeni. Oller (1971) anasema kwamba, umilisi wa imla unaonyesha umilisi wa lugha kwa ujumla; yaani msamiati, lugha, insha na matamshi. Kwa hivyo, imla inahusisha stadi zote kijumla na haipaswi kuchukuliwa kama kusoma tu kwa sauti kwa mwalimu na kuandika kimyakimya kwa mwanafunzi. Kulingana na silabasi ya Kiswahili (KIE, 2005), hivi sasa somo

la imla linafunzwa kwenye shule za msingi na za sekondari. Somo hili limeratibiwa katika stadi ya kuandika na mazoezi yake yananuiwa kuboresha stadi za kuandika na kuzungumza kwa ujumla. Sehemu hii imeeleza historia ya somo la imla. Sehemu inayofuata imechunguza jinsi somo la imla linavyoimarisha stadi ya kuandika.

## 2.3 Uimarishaji wa Stadi ya Kuandika Kupitia Somo la Imla

Utafiti wa nyanjani ulidhihirisha vipengele vya stadi ya kuandika kama vile tahajia, uakifishaji, sarufi, msamiati na hati vinavyoboreshwa na somo la imla. Vipengele hivyo vilijidhihirisha katika mahojiano na walimu na wakati wa uchunzaji wa darasani. Ili kufahamu mazoezi yanayotumiwa na walimu kukuza stadi ya kuandika, mtafiti aliwauliza walimu mazoezi waliyotumia kufundisha na kuimarisha stadi ya kuandika. Miitikio ya walimu imedokezwa katika Jedwali la 2.1.

**Jedwali la 2.1: Mazoezi yanayotumiwa kuimarisha stadi ya kuandika**

| ZOEZI | IDADI YA VIPINDI | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Insha | 5 | 50 |
| Ufahamu | 2 | 20 |
| Imla | 2 | 20 |
| Muhtasari | 1 | 10 |

Jedwali la 2.1 linaonyesha kuwa walimu walifunza somo la insha asilimia 50 ya vipindi vilivyotengewa stadi ya kuandika. Masomo ya imla na ufahamu yalichukua vipindi viwili (20%) kwa muhula. Mazoezi ya muhtasari nayo yalifanywa mara moja tu kwa muhula.

Maazimio ya kazi ya takriban walimu wote waliochunzwa yalionyesha kuwa walifunza vipindi kumi vya stadi ya kuandika katika muhula mmoja. Walimu wote 10 (100%) walisema kuwa wanatumia mazoezi ya insha kwa kiwango kikubwa kuboresha stadi ya kuandika. Kati ya masomo kumi ambayo walikuwa wameratibu kufunza kwa muhula, walifunza insha mara tano. Walimu hawa walitoa sababu kuwa somo la insha lina alama nyingi katika mtihani wa kitaifa (KCSE) kuliko masomo mengine ya kuandika.

Walimu wanane (80%) walidai kuwapa wanafunzi wao mazoezi ya imla mara mbili tu kwa muhula kwa sababu hawana muda wa kutosha. Aidha, walitoa sababu kuwa silabasi ya Kiswahili ni pana mno na hawawezi kukamilisha vipengele vyote kwa muda uliotengwa. Walimu wengine wawili (20%) walisema kuwa wanawapa wanafunzi mazoezi ya imla mara moja tu kwa muhula licha ya kuratibu mazoezi mawili katika maazimio yao ya kazi. Walimu hawa walikiri kutozingatia maazimio yao ya kazi kwa kina na wanafunza kulingana na vitabu vya kiada na miongozo ya walimu. Aidha, walimu hawa walisema kuwa somo la imla halitahiniwi moja kwa moja katika mtihani wa kitaifa kwa hivyo hawakuona haja ya kulitilia maanani.

Mazoezi mengine yaliyotajwa kuimarisha stadi ya kuandika ni ufahamu na muhtasari. Matokeo haya yanaonyesha kuwa somo la imla lilifundishwa mara chache kuliko masomo mengine. Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, mwanafunzi anapaswa kurekebishwa mara kwa mara anapofanya makosa ili ajifunze lugha, hili litawezekana ikiwa atafanya mazoezi mengi darasani.

Mtafiti alidadisi zaidi ili kufahamu kile wanafunzi walichojifunza katika kila somo la stadi ya kuandika. Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha majibu ya walimu walipoulizwa walichokusudia wanafunzi wao wajifunze katika somo la imla.

**Jedwali la 2.2: Vipengele vya stadi za lugha katika somo la imla**

| KIPENGELE | IDADI YA WALIMU | ASILIMIA |
|---|---|---|
| Tahajia | 8 | 80% |
| Sarufi | 6 | 60% |
| Hati | 7 | 70% |
| Msamiati | 5 | 50% |
| Sauti | 6 | 60% |

Jedwali la 2.2 linaonyesha kuwa asilimia kubwa ya walimu (80%) walikusudia wanafunzi wao wajifunze tahajia katika somo la imla. Walimu wengine 6 (60%) walisema kuwa somo la imla liliwasaidia kukuza sarufi ya wanafunzi. Asilimia 70 ya walimu nayo ikataja hati kama kipengele cha stadi ya kuandika walichokusudia wanafunzi wao kujifunza katika somo la imla. Msamiati na sauti ni vipengele vilivyotajwa na asilimia 50 na 60 ya walimu mtawalia. Mtafiti alitumia mbinu ya

uchunzaji wa darasani na upekuzi wa madaftari ya wanafunzi ili kuthibitisha yaliyosemwa na walimu.

Mtafiti alihudhuria madarasa mawili ya kidato cha pili katika shule tano. Lifuatalo ni jedwali linaloonyesha idadi ya wanafunzi waliochunzwa katika kila shule.

**Jedwali la 2.3: Idadi ya wanafunzi walionchunzwa**

| **SHULE** | **IDADI YA WANAFUNZI WALIOCHUNZWA** | **SAMPULI** |
|---|---|---|
| A | 98 | 20 |
| B | 103 | 21 |
| C | 84 | 16 |
| D | 92 | 18 |
| E | 77 | 15 |
| **JUMLA** | 454 | 90 |

Kulingana na Jedwali la 2.3 wanafunzi 454 walichunzwa. Kati yao, 230 (50.7%) walikuwa wasichana na 224 (49.3%) walikuwa wavulana. Baada ya uchunzaji wa darasani, mtafiti aliteua kazi za wanafunzi 90 alizotumia kuainisha makosa ya wanafunzi katika somo la imla. Katika wanafunzi 90 walioteuliwa, 44 (48.9%) walikuwa wavulana na 46 (51.1%) walikuwa wasichana.

Wanafunzi 12 (13.3%) hawakufanya makosa yoyote katika kazi zilizokaguliwa na mtafiti. Kati ya 12, 5 (5.5%) walikuwa wavulana na 7 (7.7%) wakawa wasichana.

Matokeo haya yanaonyesha kuwa wasichana walifanya vyema katika somo la imla kuliko wavulana. Isitoshe, shule za wasichana zilionekana kuwa na makosa machache kuliko za wavulana. Asilimia kubwa ya wanafunzi ambao hawakufanya makosa yoyote walitoka katika shule za kitaifa na zile za mkoa. Makosa 218 yalibainika katika kazi za wanafunzi 78. Makosa mengi, 166 (76.1%) yalikuwa ya hijai, 39 (17.9%) ya sarufi na 14 (6%) yalihusiana na maana. Aidha, wanafunzi 6 (6.7%) waliacha mapengo katika kazi zao. Wanafunzi walioacha mapengo walidai kuwa hawangeweza kumudu kasi ya mwalimu wao. Baada ya somo la imla, mtafiti alifanya mahojiano yasiyo rasmi na wanafunzi ili kufahamu kile walichojifunza katika somo la hilo. Yafuatayo ni majibu ya wanafunzi walipoulizwa kile walichojifunza katika somo la imla.

**Jedwali la 2.4: Vipengele vya Lugha ambavyo Wanafunzi Walijifunza katika Somo la Imla**

| SHULE | MAJIBU YA WANAFUNZI KABLA YA KUSAHIHISHA | MAJIBU YA WANAFUNZI BAADA YA KUSAHIHISHA |
|---|---|---|
| A | Kuwa makini, kuandika kwa kasi | Kuakifisha, kuendeleza kwa usahihi |
| B | Kuwa makini, msamiati mpya | Kuzingatia aya, kuendeleza kwa usahihi |
| C | Kuwa makini, maneno mapya | Kuandika maneno yanayosomeka, kuendeleza kwa usahihi |
| D | Msamiati mpya, kuandika kwa | Msamiati mpya, kuendeleza kwa usahihi, kutochanganya |

| | | |
|---|---|---|
| | kasi, kuwa makini | herufi |
| E | Kuwa makini, kuandika kwa kasi | Kuzingatia alama za uakifishaji, kuandika herufi ipasavyo, kuendeleza maneno kwa usahihi |

Kulingana na Jedwali la 2.4, wanafunzi wengi waliochunzwa walifikiri kuwa makini na kuandika kwa kasi kama vipengele pekee walivyojifunza katika zoezi la imla. Majibu hayo yalijitokeza kabla ya kazi zao kusahihishwa na makosa yao kubainishwa. Lakini baada ya kulinganisha kazi zao na makala asili ya mwalimu na kuchanganuliwa makosa yao na mtafiti, waliweza kubaini makosa mengine kama ya tahajia, sarufi na maana. Kutokana na uchunzaji na ukaguzi wa madaftari ya wanafunzi, mtafiti aligundua kuwa wanafunzi walijifunza kuwa makini, kuandika kwa kasi, kuandika kwa hati nadhifu, kuendeleza sauti/maneno kwa ufasaha, uakifishaji sahihi, kuzingatia ngeli na upatanisho wa kisarufi, kutamka maneno ipasavyo na msamiati mpya.

Kipengele cha pili cha Nadharia ya Uchanganuzi Makosa kiliongoza katika sehemu hii ya utafiti. Kulingana na Corder (1974), katika kujifunza lugha, mwanafunzi anaweza kufanya makosa. Makosa hayo yanapotambuliwa na kurekebishwa mara kwa mara, mwanafunzi atakuwa amejifundisha lugha. Natalicio (1979) anafananisha makosa katika mazoezi ya imla na watoto ambao katika lugha yao ya kwanza wanaweza kukariri kiapo cha utii. Uteuzi wao wa

maneno una makosa, lakini makosa yenyewe yana maana kwa watoto ambao wamezoea kutumia maneno hayo kila siku katika michezo yao. Wanafunzi hawa hawarudii tu sauti walizosikiza na kujaribu kuziiga, bali wanaunda maana kutoka kwa sauti hizo, kwa kuzibadilisha kwa kujua au kutojua ili ziwe na maana.

Makisio ya Natalicio (1979) ni kuwa haya ndiyo hufanyika wakati wanafunzi wanapojifunza lugha ya pili kila wakati. Mtafiti alitambua kwamba, makosa ambayo wanafunzi hufanya katika somo la imla yakikosolewa mara kwa mara na mwalimu, hatimaye wanafunzi wataweza kumudu vipengele mbalimbali vya stadi ya kuandika.

Kupitia uchunzaji wa darasani, mahojiano na walimu, upekuzi wa madaftari ya wanafunzi na mahojiano yasiyo rasmi na wanafunzi, mtafiti alitambua kwamba wanafunzi walijifunza yafuatayo katika somo la imla.

### 2.3.1 Tahajia

Utafiti huu ulibaini kuwa, somo la imla likifunzwa mara kwa mara na kwa utaratibu unaofaa, litawawezesha wanafunzi kutofautisha sauti mbalimbali na kuziandika ipasavyo. Kulingana na Davis na Rinvolucri (1988), kudekodi sauti na kuzirekodi katika maandishi ni hatua muhimu ya kujifunza. Katika somo la imla,

wanafunzi hurekodi sauti kutoka katika kifungu wanachosomewa na mwalimu kisha kuziandika kwa usahihi kwenye vitabu.

Mazoezi ya imla ni njia nzuri ya kufundisha tahajia kwa sababu yanaruhusu wanafunzi kuendeleza maneno katika ulimwengu halisi (Davis na Rinvolucri, 1988). Kulingana na Jedwali la 2.2, asilimia 80 ya walimu waliohojiwa walidai kuwa somo la imla linawasaidia sana kukuza tahajia ya wanafunzi, hivyo basi kuepuka makosa ya hijai. Isitoshe, mazoezi ya imla humwonyesha mwanafunzi aina za makosa ya hijai ambayo anaweza kufanya mara kwa mara. Ili kuthibitisha yaliyosemwa na walimu kuhusu uimarishaji wa tahajia ya wanafunzi kupitia somo la imla, mtafiti aliainisha makosa ya hijai yaliyofanywa na wanafunzi. Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, katika kujifunza lugha, mwanafunzi anaweza kufanya makosa, anapofanya makosa asiadhibiwe bali ichukuliwe kuwa bado hajajifunza lugha. Mwanafunzi anapaswa kurekebishwa mara kwa mara ili aweze kujifunza lugha. Kifungu cha imla kiliteuliwa na kupewa walimu wafundishie somo la imla (taz. Kiambatisho C).

Somo hili liliendeshwa kwa njia ya kawaida ambapo mwalimu aliwasomea wanafunzi makala mara ya kwanza huku wakisikiliza. Kisha mwalimu akasoma mara ya pili huku wanafunzi wakinakili waliyoyasikia. Mwalimu aliwasomea kifungu hicho tena mara ya tatu huku wanafunzi wakifanya marekebisho inapobidi. Mwalimu alipokamilisha kuwasomea wanafunzi kifungu, aliwahimiza

kuyapa makala hayo kichwa mwafaka. Baada ya somo la imla, mwalimu alikusanya vitabu vya wanafunzi na kuvisahihisha kisha kuainisha makosa mbalimbali waliyoyafanya wanafunzi. Baada ya mwalimu kusahihisha, mtafiti alichukua madaftari kadhaa ya wanafunzi akitumia mbinu bahatishi ili aweze kubainisha makosa yaliyojitokeza na kuchunguza vipengele vya stadi ya kuandika ambavyo wanafunzi walijifunza. Makosa mengi yaliyofanywa na wanafunzi yalihusiana na uendelezaji wa maneno. Baadhi ya makosa hayo ni kama vile; udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti, ubadilishaji wa sauti na kutenga silabi za neno moja visivyo.

#### 2.3.1.1 Udondoshaji wa Sauti

Udondoshaji ni hali ya kuondoa sauti kwenye silabi au neno (Massamba, 2009). Kwa mujibu wa maelezo haya, utafiti huu ulichunguza makosa ya udondoshaji wa sauti katika maneno ya Kiswahili. Uchunguzi uliofanywa unathibitisha kuwa baadhi ya wanafunzi walidondoa sauti mbalimbali. Sababu kuu ya udondoshaji ni kuwa sauti hizo hazipatikani katika lugha zao za kwanza. Sauti hizo zitokeapo katika lugha ya Kiswahili hudondoshwa ili kuchukua mtindo wa lugha zao za kwanza hivyo basi makosa yanaweza kutokea katika ujifunzaji wa L2. Baadhi ya maneno yaliyodhihirisha udondoshaji yamebainishwa katika Jedwali la 2.5.

**Jedwali la 2.5: Makosa ya Udondoshaji wa Sauti**

| Kosa | Neno Sahihi | | Kosa | Neno Sahihi |
|---|---|---|---|---|
| araka | haraka | | acha | wacha |
| nae | naye | | alipokua | alipokuwa |
| kua | kuwa | | hatimae | hatimaye |
| bio | mbio | | hakueza | hakuweza |

Jedwali la 2.5 linaonyesha kuwa wanafunzi walidondoa sauti /h/ na viyeyusho /w/ na /y/. Corder (1967) anasema kuwa, ni muhimu kutambua kiini cha makosa. Kwa mfano, kiini cha makosa kinaweza kutokana na lugha ya pili kuwa na sauti ambazo hazimo katika lugha ya kwanza. Kupitia upekuzi wa madaftari na mahojiano na walimu, mtafiti aligundua kuwa wanafunzi walifanya makosa haya kwa kuwa sauti hizi hazikuwa katika lugha zao za kwanza. Mtafiti alitambua lugha za kwanza za wanafunzi kwa kuwauliza walimu wao. Kwa mfano, mtafiti alibaini kuwa, lugha ya Kinandi na Kikamba hazina sauti /h/, kwa hivyo wazungumzaji wa lugha hizo wanapokumbana na maneno ya Kiswahili yaliyo na sauti hizo, wanazidondoa ili waweze kuyatamka kwa mfano ‘araka’ badala ya ‘haraka’. Baada ya kuchunguza udondoshaji wa sauti, sehemu ifuatayo imechunguza uchopekaji wa sauti.

### 2.3.1.2 Uchopekaji wa Sauti

Massamba (2009) anaeleza uchopekaji kama uingizaji wa sauti isiyofaa kwenye neno. Hivyo basi kwa maelezo sahili tunaweza kusema kuwa uchopekaji ni hali ambapo kitamkwa kinaingizwa katikati ya mfululizo wa vitamkwa vingine ambavyo vipo tayari katika neno. Mfanyiko huu husaidia lugha kuoanisha matamshi ya maneno na mfumo wa kifonolojia, hasa kwa kuzingatia misingi ya silabi husika. Aghalabu, vitamkwa vinavyochopekwa vinaweza kuwa na manufaa ama visiwe na manufaa, hasa pale ambapo misingi ya mfanyiko huu una asili katika L1.

Uchopekaji wa sauti mbalimbali katika maneno ya Kiswahili husababisha makosa ya hijai ambayo yanaweza kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Kazi za wanafunzi zilizokaguliwa zilionyesha wanafunzi wanachopeka sauti za nazali /n/ na /m/ katika maneno ya Kiswahili. Maneno mengi yanayopata uchopekaji huu ni yale yanaanza kwa sauti /b/, /d/ na /g/. Baadhi ya maneno yaliyoongezewa sauti yamedokezwa katika Jedwali la 2. 6.

**Jedwali la 2.6: Makosa ya Uchopekaji wa Sauti**

| **Kosa** | **Neno Sahihi** | | **Kosa** | **Neno Sahihi** |
|---|---|---|---|---|
| mbara | bara | | kuwachika | kuachika |
| nzito | zito | | kumushika | kumshika |
| ndawa | dawa | | walimulaza | walimlaza |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| ngari | gari | | dakitari | daktari |
| mzingo | mzigo | | | |

Uchopekaji mwingine ulihusisha viyeyusho. Baadhi ya wanafunzi walichopeka sauti /w/ kabla ya silabi ambazo zilikuwa na irabu pekee kwa mfano waliandika ‘kuwachika’ badala ya ‘kuachika’. Aidha, wanafunzi wengine walichopeka irabu mwishoni mwa silabi ambazo zilikuwa na muundo wa konsonanti pekee. Lugha za Kibantu huwa na silabi wazi. Kwa hivyo, baadhi ya wazungumzaji wanapokumbana na silabi funge, wanaisimilisha kwa kuongeza irabu ili iwe silabi wazi. Kwa mfano, wanafunzi wawili waliandika ‘kumushika’, badala ya ‘kumshika’. Mtafiti alibaini kuwa baadhi ya walimu waliendeleza neno hilo jinsi wanafunzi walivyoandika, yaani ku-mu-shi-ka hivyo kuchangia makosa ya uchopekaji wa irabu /u/. Sehemu inayofuata imechunguza makosa ya ubadilishaji sauti yaliyofanywa na wanafunzi.

#### 2.3.1.3 Ubadilishaji wa Sauti

Hii ni mbinu ambapo sauti ambayo haipatikani katika mfumo wa lugha fulani inabadilishwa na sauti nyingine au sauti inayokaribiana nayo (Massamba, 2009). Hali hii imetokea katika maneno mengi ya Kiswahili katika kazi za wanafunzi

zilizochunguzwa na mtafiti. Jedwali la 2.7 linaonyesha makosa ya ubadilishanaji wa sauti.

**Jedwali la 2.7: Makosa ya Ubadilishaji wa Sauti**

| **Kosa** | **Neno Sahihi** | | **Kosa** | **Neno Sahihi** |
|---|---|---|---|---|
| choka | shoka | | akivevesuka | akiwewesuka |
| Shaza | Chaza | | mziko | mzigo |
| semeji | shimeji | | anapala | anapara |
| chali | shali | | Jaza | Chaza |
| paja | pacha | | Kazi | kasi |

Jedwali la 2.7 linaonyesha kwamba sauti /sh/ /ch/ na /s/ zilibadilishana nafasi katika baadhi ya kazi za wanafunzi. Wanafunzi waliobadilisha sauti /ch/ na /sh/ walikiri kuathiriwa na lugha zao za kwanza ambapo sauti hizi hubadilishana nafasi mara kwa mara hasa zinapofuatana katika sentensi. Iliibuka katika utafiti huu kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuona tofauti ya sauti hizo mbili hata baada ya kurekebishwa na mwalimu. Wanafunzi kama hawa wanahitaji mazoezi zaidi ili waweze kumudu sauti hizo. Kulingana na Nadharia ya uchanganuzi Makosa, makosa yanaporekebishwa mara kwa mara, mwanafunzi atakuwa amejifunza lugha.

Baadhi ya wanafunzi walibadilisha sauti /j/ na /ch/ kwa mfano waliandika ‘paja’ badala ya ‘pacha’. Isitoshe wengine walibadilisha kiyeyusho /w/ na kikwamizo /v/ kama ilivyojitokeza katika neno ‘akivevesuka’ badala ya ‘akiwewesuka’. Kosa lingine lilihusu ubadilishanaji wa kitambaza /l/ na kimadende /r/ kama ilivyobainika katika neno ‘anapala’ badala ya ‘anapara’. Ilikuwa dhahiri kwa mtafiti kuwa makosa ya ubadilishanaji wa sauti yalikuwa na uzito kuliko makosa mengine ya hijai kwa sababu yalifanya maneno kubadilisha maana kabisa hivyo basi baadhi ya sentensi zikakosa mantiki. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika ‘alijifungua watoto paja’ badala ya ‘alijifungua watoto pacha’. Sentensi ya kwanza ina kosa la kimantiki ambalo limesababishwa na kosa la hijai. Makosa ya ubadilishaji wa sauti yalijitokeza katika sauti tofauti tofauti, thibitisho kuwa eneo la utafiti lilikuwa na wenyeji wenye L1 mseto. Baada ya kuchunguza makosa ya ubadilishaji sauti, sehemu ifuatayo imechunguza makosa ya utengaji silabi yaliyofanywa na wanafunzi.

#### 2.3.1.4 Kutenga Silabi

Utengaji wa silabi visivyo katika neno ni kosa la hijai. Kazi nyingi za wanafunzi zilidhihirisha makosa yafuatayo ya kutenga silabi katika maneno ya Kiswahili.

**Jedwali la 2.8: Utengaji wa Silabi**

| **Kosa** | **Neno Sahihi** |
|---|---|
| haku weza | hakuweza |
| wali mlaza | walimlaza |
| walio ifunga | walioifunga |
| wana Kijiji | wanakijiji |

Jedwali la 2.8 linaonyesha baadhi ya maneno yaliyotenganishwa na wanafunzi. Maneno mengi yaliyotengwa visivyo ni vitenzi na nomino ambata. Kati ya vitabu 90 vya wanafunzi vilivyopekuliwa, wanafunzi 30 walifanya makosa ya utengaji silabi visivyo. Baadhi ya makosa hayo yalisababishwa na kuandika haraka haraka lakini wanafunzi wengine walitenga silabi kwa sababu hawakufahamu jinsi ya kuendeleza maneno hayo. Mazoezi ya imla mara kwa mara yanaweza kuwa njia bora ya kurekebisha makosa kama haya ya kutenga silabi.

Mtafiti alibaini kuwa, wanafunzi wanapolinganisha waliyoandika na majibu sahihi katika zoezi la imla, huwaongoza jinsi ya kuboresha tahajia yao. Hata hivyo, Frodesen (1991) anasema kuwa, hakuna uhakika kuwa wanafunzi watafanya mazoezi haya nje ya darasa, lakini inatarajiwa kuwa, wakiona kuwa matokeo ya

mazoezi ya imla ni chanya darasani, watajibidiisha na kufanya mazoezi zaidi. Aidha, kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa, mwanafunzi anapokosolewa mara kwa mara, atakuwa amejifunza lugha. Sehemu ifuatayo imechunguza makosa ya sarufi yaliyofanywa na wanafunzi.

### 2.3.2 Sarufi

Mazoezi ya imla yanaweza kuwa njia bora ya kushughulikia makosa ya sarufi katika maandishi ambayo yanaweza kutokea wakati mwanafunzi anapokosa kupata dhana fulani kwa usahihi inapotamkwa (Frodesen, 1991). Asilimia 60 ya walimu waliohojiwa walidai kuwa mazoezi ya imla huwasaidia kurekebisha makosa ya sarufi ya wanafunzi. Utafiti huu ulibaini kuwa makosa ya sarufi hujitokeza kwa wingi walimu wanapofundisha imla kwa njia mseto. Makosa hayo ni pamoja na matumizi mabaya ya herufi kubwa, uakifishaji usiofaa na makosa yanayohusiana na ngeli za Kiswahili.

Uchunguzi wa kazi za wanafunzi ulidhihirisha makosa ya sarufi. Baadhi ya makosa hayo ni kutumia herufi ndogo na kubwa visivyo. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi walianza sentensi kwa herufi ndogo na kuweka herufi kubwa katikati ya neno. Upatanisho wa kisarufi pia ulikuwa tatizo katika baadhi ya sentensi za wanafunzi. Aidha, wengine hawakuweka kikomo baada ya sentensi. Mifano ya makosa ya kisarufi imebainishwa katika Jedwali la 2. 9.

**Jedwali la 2.9: Makosa ya Sarufi**

| **Kosa** | **Neno Sahihi** |
|---|---|
| kUmshIka | Kumshika |
| alIgUndUa | Aligundua |
| chaza | Chaza |
| samaki ya | samaki wa |

Kulingana na Jedwali la 2.9, makosa mengi ya sarufi yalitokana na uakifishaji usiofaa. Kwa mfano wanafunzi wanane kati ya tisini walianza neno 'chaza' kwa herufi ndogo ilhali ni nomino ya pekee. Aidha, kazi nyingi za wanafunzi zilizopekuliwa zilionyesha kuwa wanafunzi wengi walitatizika kuandika herufi *u* na *i* ndogo hivyo basi kuandika kama *U* na *I* na kusababisha makosa ya sarufi. Makosa mengine ya sarufi yalihusu upatanisho wa sarufi. Wanafunzi watatu waliandika 'samaki ya' badala ya 'samaki wa', dhihirisho kuwa hawakufahamu ngeli ya neno 'samaki'. Makosa kama haya yakitambuliwa na mwalimu na kurekebishwa mara kwa mara basi mwanafunzi anaweza kuboresha matumizi ya lugha kwa kuondoa makosa ya sarufi.

Kutokana na uchunzaji na ukaguzi wa vitabu, mtafiti alitambua kuwa somo la imla huwawezesha wanafunzi na walimu kutambua makosa yanayotokana na ufahamu

wa wanafunzi; aidha ya mofimu au sarufi. Katika Kiswahili, makosa halisi ni kama kuachwa nje au kutenga mofimu zilizo pamoja, kwa mfano kuandika *ma ma* badala ya *mama* au *mutasari* badala ya *muhtasari*. Kulingana na silabasi ya Kiswahili (KIE, 2005), uwezo wa kutambua na kubainisha vipengele vilivyotajwa hapo juu unapaswa kupatikana kufikia mwisho wa kidato cha kwanza, lakini utapata wanafunzi wakiendeleza makosa haya katika madarasa ya juu. Isitoshe, utafiti huu ulithibitisha kuwa, makosa ya tahajia yanaweza kusababisha makosa ya sarufi. Kwa mfano, neno 'mama' lisipoendelezwa ipasavyo, kosa la tahajia litajitokeza na hatimaye kanuni za sarufi kuvunjwa kwani mofimu huru huwa imetenganishwa.

Kati ya walimu sita (60%) waliotaja kipengele cha sarufi, wanne walisema kuwa mazoezi ya imla yanawasaidia wanafunzi wao kupambanua sentensi zenye utata. Mtafiti alibaini kuwa upambanuzi huo unawezekana kwa kutumia alama za uakifishaji zinazofaa, kiimbo na shadda ipasavyo, na pia kufahamu msamiati, vitawe na vitate katika sentensi zenye utata. Isitoshe, utafiti huu ulionyesha kuwa mazoezi ya imla pia husaidia wanafunzi kufahamu miundo sahihi ya sentensi. Kuna sentensi ambazo ni sahihi kisarufi, lakini sio katika muundo unaofaa, au kisemantiki hazileti maana. Kwa mfano; *Mtoto alikula meza*. Sentensi hii imezingatia kanuni zote za kisarufi lakini haileti maana katika hali halisi. Walimu waliotoa maoni haya walikuwa wa shule za kitaifa na za mkoa. Aidha, walimu hao walidai kuwa wengi wa wanafunzi wao ni wa upeo wa juu na waliwapa mazoezi

ya kuwafikirisha ili wasihisi ukimwa. Sehemu ifuatayo imechunguza jinsi hati ya mwanafunzi inavyoimarishwa na somo la imla.

### 2.3.3 Hati

Hati ni mwandiko au maandishi ya mkono, (TATAKI, 2013). Walimu saba (70%) kati ya waliotafitiwa walitumia somo la imla kuimarisha hati ya wanafunzi. Kando na lugha ya Kiswahili, wanafunzi katika shule za upili hujifunza masomo mengine ambayo hutakiwa kuendelezwa kwa hati inayosomeka. Kulingana na Davis na Rinvolucri (1988), licha ya kuwa mwanafunzi hapaswi kunakili kila kitu anachosema mwalimu katika masomo mengine, kujifunza jinsi ya kuandika lugha zungumzi kwa haraka ni mojawapo ya stadi muhimu kwa wanafunzi wa sekondari na vyuo. Kwa hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi wakipewa mazoezi ya imla huweza kuboresha hati zao wanapoandika Kiswahili na masomo mengine.

Mtafiti alitambua kwamba katika shule moja kati ya tano zilizochunzwa, zaidi ya asilimia 90% ya wanafunzi waliochunzwa waliandika kwa mwandiko uliokaribia kufanana. Hati zao zilisomeka vizuri na zilivuta makini ya mtafiti kutaka kujua zaidi. Walimu wa Kiswahili katika shule B walisema kuwa, wanatilia mkazo hati katika kidato cha kwanza na cha pili kwani kazi ya wanafunzi ikisomeka kwa haraka haitawapa ugumu wa kusahihisha. Hati ni kipengele muhimu cha stadi ya kuandika hasa katika somo la insha. Aidha, ripoti za kila mwaka za KNEC zinaorodhesha hati zisizosomeka kama mojawapo ya matatizo ya wanafunzi katika

mtihani wa kitaifa wa KCSE (KNEC, 2006-2017). Licha ya kuwa hati haitahiniwi katika mtihani wa kitaifa, inatatiza kasi ya watahini na mwanafunzi anaweza kuhiniwa alama kwa sababu ya kazi yake kutosomeka vizuri. Baada ya kuchunguza jinsi hati ya mwanafunzi inavyimarishwa na somo la imla, sehemu ifuatayo imechunguza jinsi msamiati unakuzwa kwa kutumia mazoezi ya imla.

### 2.3.4 Msamiati

Kati ya walimu 10 waliohojiwa, watano (50%) walikiri kutumia mazoezi ya imla kuimairisha msamiati wa wanafunzi. Walimu hawa walichopeka msamiati katika sentensi au vifungu walivyowasomea wanafunzi na kueleza maana ya msamiati huo baada au kabla ya zoezi. Mtafiti alibaini kupitia uchunzaji wa darasani kuwa wanafunzi walikuwa makini zaidi walipong’amua kuwa kulikuwa na msamiati mpya katika kifungu walichosomewa. Kulingana na Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano, muktadha unapaswa kupewa nafasi muhimu katika ufundishaji. Kwa mfano, msamiati mpya unaweza kuwekwa katika muktadha wa sentensi au makala. Kwa hivyo, mwalimu anapoteua makala ya kuwasomea wanafunzi, anapaswa kuhakikisha kuna msamiati mpya ili wanafunzi waweze kujifunza. Utafiti huu uligundua kwamba, mazoezi ya imla huimarisha matumizi ya msamiati kwani mwalimu anapoteua kifungu cha kuwasomea wanafunzi, yeye huchopeka msamiati anaokusudia kuwafundisha wanafunzi.

### 2.3.5 Sauti

Walimu sita (60%) walitaja sauti kama mojawapo ya kipengele walichotarajia wanafunzi kupata katika somo la imla. Walimu hawa walisema kuwa wao huteua maneno yanayowakanganya wanafunzi kutamka na kuendeleza kisha wanayatamka ipasavyo na kuwaambia wanafunzi kuyaendeleza. Walimu watano walisema kuwa wao hutumia somo la imla kuwawezesha wanafunzi kuendeleza sauti mbalimali na kutofautisha sauti tatanishi katika maneno kama vile, *thamini* na *dhamini*. Walimu waliotaja kipengele cha sauti katika somo la imla walikuwa wa shule za kutwa na zile za kibinafsi. Walitoa sababu kuwa wengi wa wanafunzi wao wana matatizo ya kuandika sauti za Kiswahili hivyo basi inawabidi walimu kutamka sauti mbalimbali huku wakiendeleza. Aidha, walimu wawili walisema kuwa wao huwauliza wanafunzi walio na matatizo ya matamshi kuwatamkia wengine kwenye vikundi darasani kisha wanaweza kuwakosoa na kuwaeleza jinsi matamshi sahihi yanapaswa kuwa. Isitoshe, katika matamshi ya maneno, walimu walitaja kusisitiza shadda na kiimbo katika maneno ya Kiswahili ili kuleta maana tofauti.

## 2.4 Uchanganuzi wa Matokeo ya Zoezi la Imla

Kabla ya kusoma zoezi la wanafunzi la imla, mtafiti alitambua kwamba baadhi ya wanafunzi hawakuandika kichwa kwa herufi kubwa na wengine hawakuzingatia pambizo katika maandishi yao. Jambo hili wamelisoma mara kwa mara na hata katika mazoezi mengine wamekuwa wakiandika wakizingatia pambizo.

Wanafunzi wengine walimaliza sentensi ghafla na kuanza nyingine. Aidha, wengine hawakuwa makini katika kuzingatia aya. Utafiti huu ulibaini kuwa, katika kuandika zoezi la imla, kukosa kusikiliza maneno mengine na kuacha nafasi wanapoandika ili kujaza baadaye kuliwafanya wasizingatie pambizo. Mtafiti alitambua kwamba, ingawaje makala yaliyosomewa wanafunzi ni sahihi kisarufi, baadhi ya wanafunzi walisikia tofauti na kuandika katika miundo tofauti.

Mtafiti alitambua kwamba wanafunzi waliofanya makosa ya msamiati hawakufahamu baadhi ya maneno yaliyotumiwa katika makala hivyo basi hawakuweza kuyachopeka kwa usahihi katika kifungu walichoandika. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika: Walimlaza *shali* na kumpepea kwa *chali* waliyoifungua kutoka kichwani pa Chaza. Ingawaje mwanafunzi huyu alisikia sauti zinazokaribiana na zile alizoandika, hangeweza kutambua kwa usahihi msamiati uliotumiwa na maana yake. Aidha, mwanafunzi mwingine hakufahamu neno ‘kicha’, badala yake aliandika neno ‘tita’. Mtafiti aling’amua kuwa, huenda ubongo wake ulinakili sauti hizo na kuzirekodi katika maneno aliyoyaelewa. Mtafiti aligundua kwamba, baadhi ya wanafunzi walifanya makosa katika maneno ambayo hayakuwa ‘mitego’ ya mwalimu. Kwa mfano, aliandika *mzingo* badala ya *mzigo*, *nzito* badala ya *zito* na *ambari* badala ya *habari*. Mtafiti alibaini kuwa hili si tatizo la kutofahamu msamiati tu, au tatizo la hijai lakini ni dhahiri kuwa mwanafunzi huyu ana tatizo la kutofautisha sauti /ng/ na /g/ inayochangia yeye kuandika neno *mzingo* badala ya *mzigo*. Aidha, huenda ameathiriwa na lugha yake

ya kwanza ya kikamba ambapo ving'ong'o hutangulia baadhi ya konsonanti kama vile /g/ na /b/.

Kutotambua msamiati halikuwa kosa pekee katika maandishi ya wanafunzi. Baadhi ya wanafunzi hawakufahamu jinsi ya kukamilisha sentensi na uakifishaji bora. Kwa mfano, katika kielelezo 1, aya ya pili, mwanafunzi mmoja alikosa kufahamu mwisho wa sentensi ya kwanza na kuweka kikomo baada ya neno *ingawa*. Isitoshe, baada ya kikomo hakuanza sentensi iliyofuata kwa herufi kubwa. Kwa hivyo, mwanafunzi huyu anakanganywa na muundo sahili wa sentensi na jinsi ya kuunda sentensi kamilifu za Kiswahili. Aidha, mwanafunzi mwingine hakutumia alama zozote za uakifishaji. Kwake, kifungu alichosomewa na mwalimu kilikuwa sentensi moja ndefu.

Baada ya mtafiti kuonyesha wanafunzi aina za makosa waliyofanya, baadhi yao walifikiri makosa yote waliyofanya yalikuwa ya hijai, ingawa baadhi yalikuwa ya sarufi na mengine yalihusu maana. Lakini ilibainika kuwa zaidi ya asilimia 50 ya makosa yalikuwa ya hijai na wanafunzi wengi wangeainisha makosa yao. Makosa ya hijai yaliyojitokeza yalikuwa ya kutenga silabi katika maneno, kubadilisha sauti na kuandika herufi visivyo. Aidha, wanafunzi wengi hawangeweza kutofautisha herufi kubwa na ndogo. Kwa mfano, herufi u iliwakanganya wanafunzi wengi walioiandika kama U bila kugundua kuwa hilo ni kosa la kisarufi. Herufi zingine ambazo hazikuandikwa kwa usahihi ni; i, j, k, w na m. Hata baada ya kuandikiwa

herufi kubwa na ndogo ubaoni, bado kulikuwa na wanafunzi ambao hawangeweza kutofautisha herufi hizo katika kazi zao. Wanafunzi kama hawa wanahitaji mazoezi ya ziada ili waweze kung'amua jinsi ya kutofautisha herufi kubwa na ndogo. Ilibainika kwamba baadhi ya walimu waliochunzwa waliendeleza herufi visivyo ubaoni bila kufahamu huku wakiwataka wanafunzi wao waendeleze herufi hizo kwa usahihi vitabuni. Swali alilojiuliza mtafiti ni, je mwalimu huyo angetambuaje makosa ya hijai na sarufi katika kazi za wanafunzi ikiwa mwenyewe anafanya makosa hayo? Utafiti huu ulibaini kuwa walimu wanahitaji kuandaa baadhi ya masomo ambayo watachunzwa na walimu wenzao ili waweze kurekebishana wenyewe.

Zoezi ambalo wanafunzi walifananisha kazi zao na makala asilia ya mwalimu lilipanua uwezo wao wa kufikiri. Awali, walikuwa wakifikiri 'kosa lingine limetokea', lakini sasa waliweza kutafakari 'Ni aina gani ya kosa?' Zoezi hili lilifanya wanafunzi kutathmini aina ya makosa waliyofanya na kuona yale waliyorudia kila mara. Mtafiti alibaini kuwa, wanafunzi wakifanya mazoezi mengi kama haya, wanaweza kufahamu zaidi kategoria za makosa wanayofanya na kuwa makini katika kutambua maneno elekezi katika zoezi la imla na maandishi kwa jumla kwa kung'amua mitego katika sentensi. Mwanafunzi anaweza kutumia mada, msamiati unaoingiliana na ukubaliano wa kiima-kiarifa ili kutambua sauti katika mazungumzo na kutambua ambapo neno au fungu la maneno halileti maana, kisha kufikiri sauti nyingine zinazokaribiana na kuingiliana kisarufi.

Kulingana na utafiti huu, somo la imla linapaswa kuwa zoezi linaloendelea. Kwanza wanafunzi watambue makosa wanayofanya, kisha wawe makini katika sehemu ambazo ziliwasumbua katika mazoezi ya imla yaliyofuata. Hizi ni hatua zinazoendelea na kukuza uwezo wa mwanafunzi wa kukuza stadi za lugha na ni zaidi ya dakika chache tu za mazoezi ya imla ya kutambua makosa na kuyachanganua katika lugha ya pili. Fischer (2003) anasema kuwa, ingawa makosa katika zoezi humuonyesha mwalimu umilisi wa lugha wa mwanafunzi, ni vyema wanafunzi kutambua makosa yao wenyewe, wajifunze umilisi wao wa lugha na udhaifu wao ili waweze kujirekebisha ndani na hata nje ya darasa. Somo la imla na uchanganuzi wa zoezi la imla unaweza kuwa kifaa muhimu katika uchanganuzi huu.

## 2.5 Hitimisho

Kutokana na uchunzaji wa darasani na usasanyuaji wa data iliyotokana na kauli ‘unakusudia wanafunzi kujifunza vipengele vipi vya stadi ya kuandika katika somo la imla’, utafiti huu umeafiki lengo la kwanza. Mtafiti amebainisha vipengele vitano vya stadi ya kuandika ambavyo wanafunzi hujifundisha katika somo la imla. Vipengele hivyo ni tahajia, sarufi, msamiati, hati na sauti. Aidha, utafiti huu umethibitisha kuwa, katika zoezi la imla, mwanafunzi anaweza kutambua sehemu anazofahamu vyema katika lugha, udhaifu wake katika maendelezo ya maneno, uundaji wa kiarifa, ukubaliano wa kiima-kiarifa na

miundo sahihi ya kisarufi. Sura inayofuata imechunguza jinsi walimu wanavyofundisha somo la imla na changamoto zinazowakumba katika kufundisha somo hilo.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA KUFUNDISHIA SOMO LA IMLA NA CHANGAMOTO ZINAZOKABILI WALIMU

## 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilichunguza vipengele vya stadi ya kuandika katika somo la imla kwa kina. Sura hii ina malengo mawili. Lengo la kwanza ni kuchanganua mbinu wanazotumia walimu kufundishia somo la imla na la pili ni kuchunguza changamoto wanazokumbana nazo katika ufundishaji wa somo hilo. Sura hii imefafanua mbinu mbalimbali za kufundisha somo la imla kama vile mwalimu kuwasomea wanafunzi maneno, sentensi au kifungu nao wakiendeleza, mwanafunzi mmoja kuwasomea wengine darasani au katika makundi na matumizi ya kanda za sauti. Aidha, changamoto katika ufundishaji wa somo la imla kama vile uteuzi wa matini ya kufundishia, silabasi pana na walimu kutoandaliwa vyema zimefafanuliwa.

Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano imetusaidia kutathmini mbinu za kufundisha somo la imla na miktadha ambayo walimu hutumia kufundisha somo hilo. Kulingana na nadharia hii, muktadha hupewa nafasi katika ufundishaji wa lugha na matumizi ya mbinu za kufundishia hutegemea viwango vya wanafunzi. Mtafiti alichunguza ikiwa walimu walizingatia muktadha na viwango vya wanafunzi wakiteua mbinu za kufundishia. Aidha, changamoto zinazowakabili walimu katika ufundishaji wa somo la imla zimefafanuliwa kwa misingi ya Nadharia ya Lugha ya


Mawasiliano. Mtafiti alitumia mbinu za mahojiano, uchunzaji wa darasani na mapitio ya vitabu vya kiada na madaftari ya wanafunzi ili kupata data iliyochanganuliwa katika sehemu hii. Walimu kumi walihojiwa na mtafiti ili kufahamu mbinu wanazotumia kufundisha somo la imla na changamoto wanazokumbana nazo katika ufundishaji wa somo hilo. Mbinu ya uchunzaji ilitumika kuthibitisha mbinu zilizotajwa na walimu na kuchunguza changamoto zilizojitokeza katika ufundishaji wa somo la imla. Sehemu ifuatayo imeangazia viwango vya elimu vya walimu waliofanyiwa utafiti.

### 3.1 Viwango vya Elimu vya Walimu

Shiundu na Omulando (1992) wanaeleza kuwa ingawa utekelezaji wa silabasi shuleni hutegemea mambo kama vile fedha, vifaa na wanafunzi miongoni mwa mengine, jambo lililo muhimu zaidi ni walimu. Walimu wanapaswa kuhakikisha kuwa yaliyomo kwenye silabasi yanawafikia wanafunzi bila kubagua ili kuwawezesha kupata stadi zote za lugha. Kwa kuwa walimu wana umuhimu mkubwa katika ufundishaji wa somo la imla, mtafiti alichunguza viwango vyao vya elimu. Kulingana na Ngugi (2008), ubunifu wa walimu katika mbinu za kufundishia unategemea kuhitimu kwao. Kwa hivyo, kabla ya kujadili mbinu za kufundishia, ni vyema kujadili viwango vya elimu vya walimu ili kuweka msingi wa kujadili mbinu wanazotumia kufundishia somo la imla.

Sehemu hii imetoa maelezo kuhusu viwango vya elimu vya walimu. Kiongozi cha maswali kilitumiwa kuchunguza viwango vya elimu vya watafitiwa. Mtafiti aliwauliza walimu kiwango cha juu kabisa cha elimu walichohitimu. Miitikio ya walimu kuhusu viwango vyao vya elimu imeonyeshwa katika Kielelezo 3.1.

**Kielelezo 3.1: Viwango vya Elimu vya Walimu**




Matokeo katika Kielelezo 3.1 yanaonyesha kuwa walimu wote 10 (100%) katika shule za sekondari walikuwa wamehitimu kufundisha Kiswahili. Ilibanika kuwa walimu 2 (20%) kati ya 10 (100%) waliohojiwa walikuwa na shahada ya uzamili, 6 (60%) walikuwa na shahada ya kwanza (Digrii) ilhali walimu 2 (20%) walikuwa na stashahada. Data hii inaonyesha kuwa, watafitiwa wote katika shule za upili walikuwa wameandaliwa kufundisha Kiswahili.

Baada ya kuelezea viwango vya elimu vya walimu, sehemu ifuatayo imeangazia ufundishaji wa stadi ya kuandika kwa jumla kwa sababu somo la imla ni mojawapo ya masomo katika stadi hii.

**3.2 Ufundishaji wa Stadi ya Kuandika**

White (1988) anasema kuwa, kuandika ni stadi muhimu kwa kuwa inatumika kukadiria kile wanafunzi wamejifundisha darasani. Kwa hivyo, stadi ya kuandika inapaswa kutiliwa maanani katika ujifunzaji na ufundishaji wa Lugha. Somo la imla limeratibiwa katika uandishi wa kawaida pamoja na ufahamu wa maandishi na muhtasari. Silabasi ya Kiswahili (KIE, 2005) imeorodhesha malengo ya stadi ya kuandika yafuatayo:

i) Kuandika hati nadhifu zinazosomeka
ii) Kuandika miundo sahihi ya sentensi
iii) Kuakifisha maandishi ipasavyo
iv) Kuzingatia tahajia sahihi katika maandishi

Silabasi ya Kiswahili (KIE, 2005) inapendekeza kuwa, azma ya kufundisha stadi ya kuandika ni kumwezesha mwanafunzi kuandika hati nadhifu na sentensi sahihi katika tungo mbalimbali. Kwa hivyo kulingana na silabasi hiyo (KIE, 2005), mwalimu amuhusishe mwanafunzi katika kuandika muhtasari, nukuu, imla, majadiliano na kudondoa hoja na fani katika maandishi. Aidha, silabasi hiyo imependekeza mafanani, vielelezo, picha, michoro, mikusanyo ya matini, vinasa

sauti, tarakilishi, maleba, mabango na vitu halisi kama nyenzo zinazoweza kutumiwa na walimu kufanikisha ufundishaji wao. Tathmini inaweza kufanywa kupitia kwa maswali ya muktadha, kujaza ufahamu, insha, kazi mradi, uchunguzi na utazamaji wa utendaji.

Benaars, Otiende na Boisvert (1994) wanasema kuwa, mbinu inayofikia malengo na ambayo haimfanyi mwalimu kuchoka ni mbinu nzuri ya kufundisha. Wanaongeza kusema kwamba, mbinu nzuri za kufundishia zinapaswa kuzingatia viwango tofauti vya wanafunzi. Asilimia 70 ya walimu waliohojiwa walisema kuwa wanazingatia uwezo na viwango tofauti vya wanafunzi kabla ya kuandaa mada za kufundisha. Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano inatilia mkazo wazo hili kwamba mada za kufundishwa darasani ziandaliwe kwa kuzingatia uwezo wa mwanafunzi. Mbinu za kufundishia zinategemea mada zinazofundishwa kwa kiasi kikubwa kama mtafiti alivyotambua katika uchunzaji wa darasani. Kwa mfano, maneno yaliyo na sauti changamano zilizowakanganya wanafunzi yalisomwa na kufafanuliwa na mwalimu mwenyewe lakini maneno ambayo hayakuwa na ugumu wowote kwa wanafunzi wengi yaliachiwa wanafunzi hao kusomeana darasani. Aidha, utafiti huu uligundua kwamba wanafunzi katika shule za kitaifa walisomewa sentensi na vifungu vilivyo changamano kuliko wanafunzi katika shule za kaunti ndogo

Baada ya kuelezea mbinu za kufundishia stadi ya kuandika kwa ujumla, sehemu ifuatayo imechunguza mbinu za kufundishia somo la imla kwa kina. Somo la imla ni mojawapo ya masomo katika stadi ya kuandika na baadhi ya mbinu za kufundisha ni mahsusi kwa somo hilo pekee.

### 3.3 Ufundishaji wa Somo la Imla

Walimu kumi wa kidato cha pili walihojiwa na mtafiti kuhusu mbinu walizotumia kufundisha somo la imla. Kupitia mahojiano na walimu na uchunzaji wa darasani, ilibainika kwamba kuna mbinu nyingi za kufundishia somo la imla. Mbinu hizo ni kama vile mwalimu kusoma kifungu huku wanafunzi wakiendeleza, mwanafunzi mmoja kusomea wengine darasani, wanafunzi kusomeana katika vikundi na matumizi ya kanda za sauti. Utafiti huu uligundua kuwa walimu hutumia mbinu mbalimbali zinazowawezesha kufanikisha somo la imla kando na ile iliyodokezwa katika vitabu vya kiada. Quist (2000) anasema kuwa, walimu hutumia mbinu zilizoorodheshwa vitabuni kwa wingi kuliko mbinu wanazobuni wenyewe. Mtafiti alichunguza kitabu cha kiada (KLB, 2018) kilichopendekezwa na Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa Nchini Kenya (K.I.C.D). Kitabu hicho kinapendekeza mbinu ifuatayo itumike katika ufundishaji wa somo la imla:

- Mwalimu awasomee wanafunzi makala mara ya kwanza huku wakisikiliza.
- Mwalimu awasomee mara ya pili huku wanafunzi wakinakili wanayoyasikia.

- Mwalimu awasomee mara ya tatu huku wakifanya marekebisho inapobidi.
- Mwalimu asahihishe kazi zao.
- Wanafunzi wenye udhaifu waandaliwe mazoezi ya ziada.

Utafiti huu ulithibitisha madai ya Quist (2000) kwamba walimu wengi huegemea mbinu zilizodokezwa vitabuni. Walimu 9 (90%) kati ya 10 (100%) waliohojiwa walisema kuwa wanapendelea kutumia mbinu iliyodokezwa katika kitabu cha kiada (KLB, 2018) ya kuwasomea wanafunzi nao wakiendeleza. Kwa mujibu wa Ornstein (1995), mbinu mbalimbali zinapaswa kutumiwa katika mazingira na viwango tofauti vya wanafunzi ili kufanikisha ufundishaji. Hili husababisha walimu kubuni mbinu mbalimbali za kufundishia ili kutekeleza mahitaji ya wanafunzi wao. Kupitia uchunzaji wa darasani na mahojiano na walimu, mtafiti alibaini mbinu tofauti ambazo hutumiwa na walimu kufundishia somo la imla ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi wao.

Walimu waliofanyiwa utafiti walitumia mada tofauti za kufundisha kutegemea viwango vya wanafunzi wao. Kwa mfano, katika shule za kitaifa na zile za mkoa, walimu waliteua vifungu changamano vilivyo na msamiati mpya lakini katika shule za kaunti ndogo walimu walitumia sentensi sahili kufundisha imla. Walimu wa shule za kitaifa na mkoa walisema kuwa, sababu ya kuteua vifungu changamano ni kuwa wanafunzi wao walikuwa wapevu na walihitaji zoezi la

kuwafikirisha zaidi ili wawe makini katika somo. Jedwali la 3.1 linaonyesha mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha somo la imla.

**Jedwali la 3.1: Mbinu zinazotumiwa na walimu kufundishia somo la imla**

| **Mbinu za kufundisha** | **Miitikio ya Walimu** | | **Jumla** |
|---|---|---|---|
| | **Waliotumia Mbinu** | **Wasiotumia mbinu** | |
| Mwalimu kusoma na wanafunzi wakiandika | 9 (90%) | 1 (10%) | 10 (100%) |
| Mwanafunzi kusoma mbele ya darasa na wengine wakiandika | 3 (30%) | 7 (70%) | 10 (100%) |
| Mwanafunzi mmoja kuwasomea wengine katika kikundi | 1 (10%) | 9 (90%) | 10 (10%) |
| Kanda za sauti | 1(10%) | 9 (90%) | 10 (10%) |

Kulingana na Jedwali la 3.1, walimu 9 (90%) kati ya 10 (100%) waliohojiwa walipendelea mbinu iliyodokezwa katika kitabu cha kiada (KLB, 2018) inayoeleza kwamba mwalimu awasomee wanafunzi maneno, sentensi au kifungu nao wanafunzi wakiendeleza. Walimu waliopendelea mbinu hii walidai kuwa mbinu hii huwasaidia kuweka mazingira yanayofaa kwa sababu wao ndio wanaowaelewa wanafunzi wao vyema. Davis na Rinvolucri (1988) wanasema kuwa mazingira ni muhimu na humpa motisha mwanafunzi na mwalimu anapaswa kutamka kwa namna itakayomwezesha mwanafunzi kuandika ipasavyo. Isitoshe, mwalimu asitamke haraka au kutumia misamiati mingi isiyoeleweka na wengi kwani hili litawasumbua kimawazo. Kwa hivyo, Davis na Rinvolucri (1988) wanaongeza

kwamba, ni vyema kupanga makala kulingana na uchangamano wake, pia kulingana na maneno mapya, yasiyojulikana hadi yanayojulikana. Wanafunzi wakianza kuzoea sauti na kasi watafanikiwa kwa kiasi na hii ni motisha kubwa. Utafiti huu ulitambua kwamba, walimu walioweka mazingira yanayofaa katika ufundishaji wao, walifaulu kwa kiasi kikubwa kuwasilisha somo la imla. Walimu hawa walisoma kwa mwendo wa kadri ili kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaandika waliyoyasikia. Aidha, walirudia sentensi pale ilipobidi. Baada ya kusahihisha kazi za wanafunzi, ilidhihika kuwa wanafunzi katika madarasa haya walikuwa na makosa machache ikilinganishwa na pale walimu waliposoma haraka haraka.

Kulingana na Jedwali la 3.1, walimu 3 (30%) kati ya 10 (100%) walitumia mbinu ya mwanafunzi mmoja kuwasomea wengine kifungu darasani huku wakiendeleza. Wakati wa kusoma, mwalimu alisikiliza ikiwa kuna maneno yaliyotamkwa visivyo na kuyanakili. Baadaye mwalimu alisoma kifungu ili wanafunzi wafanye marekebisho. Walimu hawa walisema kwamba walipendelea mbinu hii kwa sababu wanafunzi wanaweza kujikosoa wenyewe. Isitoshe, walimu waliotumia mbinu hii walidai kwamba inawasaidia kutathmini matamshi ya wanafunzi na tahajia yao kwa wakati mmoja. Aidha, kupitia uchunzaji wa darasani mtafiti alibaini kuwa wanafunzi wenye kasi waliweza kusaidia wengine ili wawe katika usawa.

Kulingana na Jedwali la 3.1, mwalimu mmoja (10%) kati ya 10 (100%) aliwaweka wanafunzi kwenye vikundi kisha kumchagua mwanafunzi mmoja kuwasomea wengine kwenye kikundi. Mwalimu huyu alidai kuwa mbinu hii iliwashirikisha wanafunzi wengi zaidi na ilihusisha darasa zima. Mwalimu pia alipata fursa ya kuzunguka darasani akitazama kile kila kikundi kinafanya.

Jedwali la 3.1 linaonyesha kuwa mwalimu mmoja (10%) kati ya 10 (100%) waliohojiwa alitumia kanda ya sauti kufundisha somo la imla. Baada ya kurekodi kifungu, mwalimu aliwachezea wanafunzi huku wakiendeleza wanayoyasikia. Ikiwa kuna maneno ambayo hayakusikika vyema, mwanafunzi alihitajika kusema 'rudia' kisha mwalimu alicheza sehemu hiyo tena. Mwalimu mmoja akisifia mbinu hii alisema, "*Mbinu hii inachangamkiwa sana na wanafunzi. Kilicho muhimu ni kutunga sentensi zinazowasisimua na kuwafurahisha wanafunzi. Kwa kufanya hivyo, zoezi la imla litakuwa rahisi kwao na hili litakuwezesha kutathmini vipengele kadhaa kama vile tahajia, uakifishaji na msamiati kwa kutumia sentensi chache tu. Aidha, wanafunzi wataweza kutambua makosa wanayofanya mara kwa mara na kuyarekebisha."*

Fisher (2001) anasema kuwa ufaafu wa somo la imla utategemea ubunifu wa mwalimu kwani kwa muda mrefu somo la imla limechukuliwa kuwa la kizamani. Sehemu hii imeangazia mbinu tofauti ambazo walimu wanatumia kufundisha somo la imla ili kuafikia malengo ya stadi ya kuandika. Kutokana na uchunzaji wa

darasani, mtafiti alibaini kuwa mwalimu anapaswa kuwa mbunifu ili wanafunzi wake wawe wachangamfu na wasipoteze makini.

Kupitia mbinu za uchunzaji na mahojiano na walimu, mtafiti aligundua kwamba baadhi ya walimu walifundisha somo la imla na somo lingine kwa wakati mmoja. Kwa mfano, mwalimu mmoja aliwasomea wanafunzi kifungu kutoka katika somo la Isimu Jamii. Jedwali la 3.2 linaonyesha idadi ya walimu waliotumia mbinu mseto kufundisha somo la imla.

**Jedwali 3.2: Usetaji wa Somo la Imla**

| **Ufundishaji kwa Njia Mseto** | **Miitikio ya Walimu** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Waliotumia | 8 | 80 |
| Wasiotumia | 2 | 20 |
| **Jumla** | 10 | 100 |

Jedwali la 3.2 linaonyesha kuwa walimu 8 (80%) walifundisha somo la imla kwa njia mseto. Usetaji ni mbinu ambayo masomo mawili au zaidi hufundishwa kwa wakati mmoja. Kwa mfano, somo la imla hujumuishwa na masomo mengine kama vile sarufi, fasihi au msamiati na kufunzwa kwa wakati mmoja. Kulingana na silabasi ya Kiswahili (KIE, 2005) mwalimu anapaswa kufundisha njia mseto. Asilimia 80 ya walimu waliohojiwa walisema kuwa hawawezi kuwasomea wanafunzi kifungu cha aya moja kwa kipindi kizima, sharti wafundishe na

masomo mengine kama vile matamshi, sarufi, vitate, vitawe, visawe, msamiati au fasihi. Kwa mfano, ikiwa mwalimu anataka kufundisha vitawe, anaweza kuwasomea wanafunzi sentensi au kifungu kilicho na maneno hayo kisha kuwaambia wanafunzi kueleza maana baada ya kuandika. Kama ilivyojitokeza katika kipindi kimoja, mwalimu aliseta somo la imla, vitawe na sarufi katika somo moja. Aliwasomea wanafunzi sentensi zifuatazo;

1. Jane anaishi kwenye mpaka wa Burundi na Rwanda.
2. Alimkimbiza mpaka dukani.
3. Juma ni mpaka rangi stadi sana.

Licha ya kuwa hili lilikuwa somo la imla, mwalimu alitaka kubaini ikiwa wanafunzi walielewa maana tofauti ya 'mpaka' katika sentensi tatu alizozisoma. Aidha, mwalimu alitaka kubaini ikiwa wanafunzi wangeweza kueleza maana ya kisarufi ya 'mpaka' katika sentensi hizo. Kando na kuangalia uakifishaji na matumizi ya herufi kubwa, mwalimu alichunguza tahajia ya wanafunzi. Matokeo haya ni dhihirisho kuwa somo la imla linaweza kutumika kukuza sarufi na uakifishaji kando na kukuza tahajia ya mwanafunzi.

Katika shule ya B mwalimu aliseta somo la imla na la matamshi bora. Mwalimu huyo aliwasomea wanafunzi maneno yafuatayo yenye sauti tatanishi /t/, /d/, /f/ na /v/ kama ilivyobainishwa katika Jedwali la 3.2.

**Jedwali la 3.3: Vitate Vinavyohushisha Maneno yenye Sauti f, v na t, d**

| f | v | | t | d |
|---|---|---|---|---|
| fua | vua | | toa | doa |
| fuka | vuka | | tata | dada |
| funga | vunga | | taka | daka |
| futa | vuta | | tua | dua |
| fumba | vumba | | teka | deka |
| fuma | Vuma | | tai | dai |
| | | | tunga | dunga |

Jedwali la 3.3 linaonyesha jinsi mwalimu alivyoseta somo la imla na lile la sauti tatanishi. Baada ya kuwasomea wanafunzi sauti hizo, mwalimu aliteua wanafunzi kadhaa na kuwauliza kusoma kwa sauti kile walichoandika. Baadaye aliwauliza wanafunzi kutunga sentensi zilizo sahihi kisarufi ili kudhihirisha maana ya maneno waliyosomewa. Mwalimu huyu alitumia somo la imla kufundishia sauti, matamshi na sarufi ili kukidhi malengo yake kama yalivyodokezwa kwenye maazimio yake ya kazi katika Kielelezo 3.2.

**Kielelezo 3.2: Maazimio ya Kazi, Shule B**

| JUMA | KIPINDI | SOMO | SHABAHA | MBINU | VIFAA | ASILIA | MAONI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 9 | 2 | Imla<br><br>Sauti t d, f na v | Kufikia mwisho wa funzo mwanafunzi aweze:<br><br>Kuandika maneno anayosomewa na mwalimu kwa usahihi na kwa hati nadhifu<br><br>Kutamka kwa usahihi sauti ambazo ameziandika<br><br>Kutunga sentensi zilizo sahihi kisarufi | Kusikiliza<br><br>Kuandika | Chaki<br><br>Ubao<br><br>Daftari | KLB kdt 2 uk 166<br><br>Fasaha kdt2 uk 189 | |

Kielelezo 3.1 kinadhihirisha jinsi mwalimu katika shule B alivyoseta somo la imla na lile la sauti. Malengo ya somo hili kulingana na Kielelezo 3.1 yanaonyesha kuwa mwalimu alikusudia kufundisha vipengele vingine kama vile hati, sauti na sarufi katika somo la imla. Walimu wote waliohojiwa walisema kuwa mbinu ya usetaji inawawezesha kufundisha vipengele viwili vya lugha kwa wakati mmoja hivyo basi kuokoa muda. Kwa mfano, kulingana na shabaha kwenye kielelezo 3.1, mwalimu katika shule B alifundisha matamshi sahihi na sarufi katika somo la imla. Mwalimu huyu aliposahihisha kazi za wanafunzi, alirekebisha makosa ya sarufi na tahajia yaliyojitokeza. Ilidhihirika katika utafiti huu kuwa, wanafunzi walipopewa

mazoezi yenye maneno yaliyokosolewa na mwalimu awali, walirekebisha makosa hayo. Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano hupendekeza matumizi ya lugha kwa wingi darasani kwa sababu mtu hupata umilisi bora wa lugha kwa kuitumia. Aidha, Nadharia hiyo inapendekeza kuwa, mwanafunzi anapofanya makosa akosolewe na mwalimu ili aweze kujifunza lugha kama alivyofanya mwalimu katika shule B.

Usetaji mwingine ulihusisha somo la imla na lile la msamiati. Katika darasa moja, mwalimu aliwapa wanafunzi zoezi la imla bila kuwaandaa kwa msamiati waliokumbana nao katika makala. Mwalimu huyu alikusudia kuwa huenda tatizo la uteuzi wa msamiati uliopo kwenye makala ukawapa baadhi ya wanafunzi changamoto; kama yalivyokuwa makisio yake, msamiati huo ulikanganya baadhi ya wanafunzi. Katika darasa lingine, mwalimu aliwaandaa wanafunzi kwa kuandika msamiati uliopatikana kwenye makala ubaoni na hata kueleza maana ya maneno hayo. Maneno yaliyoandikwa ubaoni ni yafuatayo: *chali*, *shali, kicha*, *kisha, para, bara*. Mwalimu huyu alikusudia wanafunzi wake wajifunze msamiati mpya kati ya vipengele vingine katika zoezi hilo la imla. Aidha, katika mojawapo ya madarasa yaliyochunzwa, mwalimu alitanguliza somo la matamshi bora kabla ya kuwapa wanafunzi zoezi la imla. Alifundisha maneno yenye sauti tatanishi /sh/ na /ch/ kabla ya kuwapa wanafunzi zoezi la imla.

Sehemu ya kwanza ya sura hii imetimiza lengo la kwanza la sura hii ambalo ni kuchunguza mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha somo la imla. Mtafiti alitambua kwamba, licha ya kuwa walimu walijitahidi kutumia mbinu mbalimbali kufundisha somo la imla, walikabiliwa na changamoto nyingi. Sehemu ifuatayo imeangazia sehemu ya pili ya lengo la sura hii ambalo ni kuchunguza changamoto zinazowakumba walimu katika ufundishaji wa somo la imla.

## 3.4 Changamoto Zinazowakumba Walimu katika Ufundishaji wa Somo la Imla

Mtafiti aliwahoji walimu kumi (100%) wa kidato cha pili ili kufahamu changamoto zinazowakumba katika ufundishaji wa somo la imla. Swali lililojibiwa na wahojiwa ni; Je, ni changamoto zipi unazokumbana nazo katika ufundishaji wa imla? Jedwali la 3.3 linaonyesha changamoto za ufundishaji zilizojitokeza katika utafiti huu.

**Jedwali la 3.4: Changamoto katika Uwasilishaji wa Somo la Imla**

| Changamoto | Idadi ya Walimu Waliotaja Changamoto | Asilimia |
|---|---|---|
| Ukosefu wa Muda wa Kutosha wa kufundisha | 10 | 100 |
| Idadi Kubwa ya Wanafunzi | 8 | 80 |
| Ugumu katika Uteuzi wa Matini ya Kufundishia imla | 7 | 70 |
| Mazoezi | 4 | 40 |
| Kutathmini Darasani | 6 | 60 |
| Ufundishaji kwa Njia Mseto | 2 | 20 |
| Silabasi Pana | 8 | 80 |
| Kutotathminiwa kwa Imla | 7 | 70 |
| Kutoandaliwa kwa walimu Ipasavyo | 5 | 50 |
| Uteuzi wa Vifaa vya Kufundishia | 4 | 40 |
| Mazingira | 2 | 20 |

Jedwali la 3.4 linaonyesha kuwa, walimu wote 10 (100%) walisema kuwa, hawakuwa na muda wa kutosha kufundisha kipengele cha imla kwa sababu ya upana wa silabasi ya Kiswahili. Tatizo hili liliwafanya kutofundisha somo la imla kwa undani.  Walimu wanne (40%) walisema kuwa, waliwaambia wanafunzi kusomeana vifungu vya imla wakati wa muda wa ziada kwa sababu ya ukosefu wa muda wa kutosha kufundisha. Walimu hawa waliongeza kuwa, kuondolewa kwa

vipindi vya ziada na serikali kumechangia kupungua kwa muda wa kufundisha masomo mbalimbali.

Walimu wawili (20%) kati ya 10 (100%) walidai kuwa walifundisha imla kwa hiari kwa sababu hawakuwa na vipindi mahsusi vya kufundishia somo la imla. Walimu wengine wanne (40%) nao walisema kuwa, waliwapa wanafunzi mazoezi ya imla yaliyoorodheshwa kwenye vitabu vya kiada tu bila kuongeza mengine ili kuokoa muda. Kauli hizi zinadhihirisha kuwa, somo la imla lilifundishwa kijuujuu licha ya somo hilo kuwa na umuhimu mkubwa katika kukuza stadi ya kuandika. Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano inadokeza kuwa lugha itumiwe kwa wingi darasani ili wanafunzi waweze kujifunza. Ukosefu wa muda wa kutosha unafanya somo la imla kutofundishwa darasani kwa upana hivyo basi kuchangia wanafunzi wasijifunze lugha ipasavyo.

Kulingana na Jedwali la 3.4, walimu 8 (80%) kati ya 10 (100%) walisema kuwa idadi kubwa ya wanafunzi iliwafanya kutosahihisha vitabu vyote kwa wakati. Walimu hawa walieleza kuwa, japo waliwapa wanafunzi mazoezi ya imla, aghalabu walikosa kusahihisha madaftari yote kwa sababu ya idadi kubwa ya wanafunzi. Tatizo hili lilichochewa zaidi na idadi ndogo ya walimu wa Kiswahili katika shule mbalimbali iliyowafanya walimu kuwa na masomo mengi kwa juma hivyo kukosa muda wa kusahihisha. Aidha, walimu hao walidai kuwa masomo ya

bure katika shule za kutwa yalichangia wanafunzi kuongezeka kiasi kwamba walimu hawawezi kuwamudu ipasavyo.

Jedwali la 3.4 linaonyesha kuwa, walimu saba (70%) kati ya 10 (100%) walitaja uteuzi wa matini kama mojawapo ya changamoto zilizowakabili katika kufundisha imla. Walieleza kuwa, vitabu vya kiada vilidokeza kuwa walipaswa kuwasomea wanafunzi kifungu bila kubainisha kifungu kitolewe kwa matini yapi. Kwa hivyo, walitatizika kuteua matini ya kuwasomea wanafunzi. Walimu watatu kati ya saba waliotaja changamoto hii walisema kuwa matini nyingi za kufundishia hazikukidhi malengo ya somo la imla kwa upana. Mwalimu mmoja alisema kuwa ilikuwa vigumu kwake kupata makala yaliyoangazia vipengele mbalimbali alivyokusudia wanafunzi wajifunze. Kwa mfano alitatizika kupata matini yenye msamiati wa magonjwa mbalimbali alipokusudia kuyatumia kufundisha somo la imla.

Kuhusu usetaji, walimu wawili (20%) walisema kuwa, walitatizika kufundisha somo la imla kwa njia mseto. Walimu hawa walisema kuwa aghalabu wao waliwasomea wanafunzi vifungu kama ilivyodokezwa kwenye silabasi au wakati wa kutanguliza somo la sauti tatanishi. Aidha, walieleza kuwa ilikuwa vigumu kwao kuseta somo la imla na masomo mengineyo kama fasihi na sarufi kwa kuwa hawakuelekezwa na silabasi na vitabu vya kiada.

Kulingana na Jedwali la 3.4, asilimia kubwa ya walimu (80%) waliohojiwa walitaja upana wa silabasi kama changamoto inayowakabili. Walimu hawa walitoa kauli kuwa kuna vipengele vingi sana katika silabasi walivyohitajika kuvishughulikia hivyo basi ni vigumu kuvikamilisha kwa muda unaofaa. Mtafiti alitambua kwamba upana wa silabasi na ukosefu wa muda wa kutosha kufundisha vipengele vyote vya silabasi ulifanya walimu kutilia mkazo masomo yanayotahiniwa katika mtihani wa kitaifa pekee. Somo la imla halitahiniwi moja kwa moja lakini linachangia vipengele vingine kama vile sarufi na tahajia ambavyo vinatahiniwa. Kwa hivyo, somo hili linapaswa kutengewa muda wa kutosha kama masomo mengine ya stadi ya kuandika kwa kuwa lina umuhimu wake.

Aidha, kulingana na Jedwali la 3.4, walimu saba (70%) walitaja kutotathminiwa kwa somo la imla kama changamoto inayowakabili. Walimu hawa walisema kuwa walizamia sehemu zilizotahiniwa kama ufahamu, insha na muhtasari. Mwalimu mmoja (10%) alidokeza kuwa yeye hutahini somo la imla japo katika maandishi ili kubaini ikiwa wanafunzi wake wanajua kuendeleza baadhi ya maneno. Kwa mfano, katika mtihani wa kidato cha pili, aliuliza swali lifuatalo: Maneno yafuatayo yameendelezwa vibaya, yasahihishe. i) Hayirisha ii) Monyonyoko iii) Tafathali iv) Jeduali. Mtafiti alitambua kwamba wanafunzi wengi katika darasa hilo walishindwa kuendeleza maneno hayo ipasavyo. Hili ni dhihirisho kuwa

maswali ya imla yakitahiniwa mara kwa mara wanafunzi wataweza kuendeleza maneno kwa usahihi.

### 3.5 Hitimisho

Sura hii imechunguza uwasilishaji wa somo la imla na changamoto zinazowakumba walimu katika ufundishaji wa somo la imla. Mbinu zilizobainishwa ni: Mwalimu kuwasomea wanafunzi, mwanafunzi mmoja kuwasomea wengine darasani, wanafunzi kusomeana katika makundi na matumizi ya tepurekoda. Ilibainika kuwa mbinu iliyotumika kwa upana ni ile iliyodokezwa katika vitabu vya kiada ya mwalimu kuwasomea wanafunzi huku wakiendeleza. Changamoto zinazowakumba walimu kama vile ukosefu wa muda wa kutosha, kutotathminiwa kwa somo la imla, upana wa silabasi na matatizo ya usetaji pia zimechunguzwa. Sura inayofuata imechanganua udhaifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla ili kutoa mapendekezo ya kuboresha somo la imla.

# SURA YA NNE

# UDHAIFU KATIKA UFUNDISHAJI NA UJIFUNZAJI WA SOMO LA IMLA

## 4.0 UTANGULIZI

Sura iliyotangulia ilichunguza mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha somo la imla na changamoto wanazokumbana nazo katika ufundishaji wa somo hilo. Ilibainika kwamba, kuna changamoto nyingi katika mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha somo la imla. Lengo la sura hii ni kubaini udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla. Sura hii imechunguza udhaifu uliojitokeza kwa walimu, wanafunzi, silabasi, vitabu vya kiada na mazingira ya darasani. Kupitia mahojiano na walimu, uchunzaji wa darasani, mapitio ya silabasi, upekuzi wa vitabu vya kiada na madaftari ya wanafunzi, mtafiti alibaini udhaifu katika uwasilishaji na upokezi wa imla ili kutoa mapendekezo.

Kupitia mhimili wa Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano kuwa ni lazima kuwe na matumizi ya lugha kwa wingi darasani, mtafiti alibaini udhaifu katika ufundishaji na upokezi wa imla. Mtafiti amebaini kuwa baadhi ya walimu wanafundisha kipengele cha imla mara moja tu kwa mwaka licha ya umuhimu wa somo hilo. Nadharia ya Uchanganuzi Makosa inapendekeza wanafunzi wakosolewe mara kwa mara ili waweze kujifunza lugha. Hili litawezekana ikiwa walimu watafundisha vipengele vyote vya stadi za lugha bila kubagua.

Sehemu ifuatayo imeonyesha udhaifu uliojitokeza wakati wa kufundisha na kujifunza imla. Mtafiti aligundua kwamba baadhi ya udhaifu uliojitokeza ulisababisha changamoto kuu na hata kutinga uwasilishaji na upokezi wa somo hilo kwa walimu na wanafunzi mtawalia. Mtafiti alikusanya data kupitia mahojiano na walimu, uchunzaji wa darasani, mapitio ya silabasi na upekuzi wa vitabu vya wanafunzi. Sehemu inayofuata imechunguza udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji wa somo la imla.

## 4.1 Udhaifu Uliojitokeza katika Ufundishaji wa somo la Imla

Matatizo katika ujifunzaji wa imla yanasababishwa na udhaifu katika ufundishaji wa walimu na ujifunzaji wa somo hilo kama ilivyojitokeza katika utafiti huu. Baadhi ya udhaifu uliibua changamoto na hata kutinga ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla.

Kupitia mbinu ya uchunzaji wa darasani, mahojiano na mapitio ya madaftari ya wanafunzi, mtafiti alibaini udhaifu uliojitokeza katika mbinu za kufundishia, matamshi ya walimu, vifaa na vitabu vya kufundishia, silabasi, uteuzi wa matini na maandalizi ya walimu. Mtafiti aliuliza walimu 10 waliochunzwa, je, unafikiri ni sababu zipi zinazofanya baadhi ya walimu wasifundishe somo la imla kwa undani? Jedwali la 4.1 linaonyesha udhaifu uliodhihirishwa na walimu kupitia mahojiano, uchunzaji wa darasani na mapitio ya madaftari ya wanafunzi.

**Jedwali la 4.1: Udhaifu katika Ufundishaji wa Imla**

| **Udhaifu Uliodhihirika katika Ufundishaji** | **Idadi ya Walimu Waliodhihirisha Udhaifu** | **Asilimia** |
|---|---|---|
| Kutumia mbinu moja kufundisha imla | 5 | 50% |
| Kutotumia vifaa vya kufundishia | 4 | 40% |
| Matamshi yasiyofaa ya walimu | 3 | 30% |
| Kutosahihisha kazi | 2 | 20% |
| Uteuzi wa Matini | 10 | 100% |
| Walimu Kutoandaliwa vyema | 5 | 50% |
| Kuweka Mazingira yasiyofaa | 2 | 20% |
| Kutoonyesha makosa katika kazi za wanafunzi | 3 | 30% |

Jedwali la 4.1 linaonyesha kuwa walimu 5 (50%) kati ya 10 (100%) waliofanyiwa utafiti walikuwa na udhaifu katika mbinu za kufundishia somo la imla. Walimu hawa walitumia mbinu moja tu kuwapa wanafunzi mazoezi ya imla. Kati ya walimu 10 (100%) waliofanyiwa utafiti, watatu (30%) walikuwa na shida ya matamshi. Walimu hawa walitamka sauti mbalimbali za Kiswahili visivyo kwa mfano /ch/ badala ya /j/ na /l/ badala ya /r/ kama ilivyodhihirika katika maneno *chaza/jaza* na *anapala/anapara*. Walimu wote 10 (100%) waliohojiwa walisema

kuwa walitatizika kuteua matini ya kufundishia somo la imla. Walimu hawa walitumia matini zilizopatikana kwenye vitabu vya kiada hasa vifungu vya ufahamu kwa wingi. Matini nyingine kutoka kwa isimu jamii, fasihi simulizi, fasihi andishi, muhtasari na insha zilipuuzwa na takriban asilimia 50 ya walimu.

Kulingana na Jedwali la 4.1, udhaifu wa vifaa na vitabu vya kufundishia ulijitokeza kwa walimu 4 (40%). Walimu wawili (20%) hawakusahihisha kazi za wanafunzi licha ya kuwapa mazoezi ya imla. Isitoshe, walimu wengine watatu walisahihisha kazi za wanafunzi bila kuonyesha makosa mahsusi yaliyofanywa na wanafunzi. Aidha, mtafiti alipowauliza walimu iwapo wamepata mafunzo yoyote katika ufundishaji wa imla alibaini kuwa walimu 5 (50%) kati ya 10 (100%) hawajapata mafunzo mengine mahsusi ya kufundisha somo la imla baada ya kukamilisha kozi zao za ualimu katika vyuo. Wao walitegemea mafunzo ya kijumla waliyopokea katika vyuo. Licha ya walimu hao kufundishwa mbinu za kufundisha somo la Kiswahili, hawakufunzwa jinsi ya kufundisha somo la imla. Kwa hivyo, ilibainika kuwa walimu hao walihitaji mafunzo mengine katika warsha na semina mbalimbali ili kupiga msasa waliyojifunza katika vyuo.

Sehemu ifuatayo imechanganua udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji wa somo la imla ili kupendekeza mbinu za kuliboresha katika sura inayofuata.

### 4.1.1 Mbinu za Kufundishia

Kulingana na Jedwali la 4.1, ilibainika katika utafiti huu kwamba walimu 5 (50%) kati ya 10 (100%) waliotafitiwa walitumia mbinu moja tu kuwapa wanafunzi mazoezi ya imla. Mbinu hii ilikuwa ya mwalimu kusoma huku wanafunzi wakiendeleza. Ni walimu 5 (50%) ambao walitumia mbinu kama vile mwanafunzi kuwasomea wengine darasani au wanafunzi kusomeana katika vikundi na tepurekoda kufundisha somo la imla. Mtafiti alitambua kuwa baadhi ya wanafunzi walikosa motisha kwa sababu waliona zoezi la imla kama la kushindana kuandika haraka haraka bila kuwa na umuhimu wowote kwao.

### 4.1.2 Mazingira ya Darasani

Jedwali la 4.1 linadhihirisha kuwa walimu 2 (20%) kati ya 10 (100%) hawakuweka mazingira yanayofaa katika uwasilishaji wa somo la imla. Kwa mfano, mwalimu mmoja (10%) alisoma kifungu kwa kasi sana na alipoulizwa kurudia alimkemea mwanafunzi na kumwambia ‘wacha kuzubaa darasani’. Kitendo hiki kiliwafanya wanafunzi wengine kuwa waoga na hawakuthubutu kulalamika tena katika somo zima kama walivyokiri kupitia mahojiano yasiyo rasmi. Udhaifu huu uliwafanya baadhi ya wanafunzi kutopata kile ambacho mwalimu alikusudia wapate kwa sababu ya kuwa waoga kama ilivyodhihirika katika madaftari ya wanafunzi kwani wanafunzi wengi walifanya makosa katika somo hili. Aidha, baadhi ya wanafunzi walikiri kuwa walifanya zoezi la imla kwa

uoga wakifikiri kuwa mwalimu alikuwa akijaribu kuwatafutia makosa ili kuwaadhibu. Davis na Rinvolucri (1988) wanasema kwamba mazingira ya darasani ni muhimu na humpa mwanafunzi motisha. Wanaongeza kuwa, mwalimu anapaswa kutamka kwa namna itakayowawezesha wanafunzi kuandika ipasavyo, mwalimu asitamke haraka kwani hili litawasumbua wanafunzi kimawazo. Aidha, utafiti huu uligundua udhaifu katika matamshi ya walimu ambao umeelezwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.1.3 Matamshi ya Walimu

Baada ya kuwahoji walimu na kusikiliza walivyofundisha darasani, mtafiti aligundua kwamba walimu 3 (30%) walikuwa na shida ya matamshi. Kulingana na Jedwali la 3.1, kati ya walimu 10 (100%) waliofanyiwa utafiti, watatu (30%) walikuwa na shida ya matamshi. Mwalimu mmoja (10%) alitatizika kutamka /l/, /r/ na /th/ na /dh/ na mwingine alikuwa na ugumu kutamka sauti /p/, /b/ na /j/, /ch/. Kwa mfano, alitamka ‘Jaza’ badala ya ‘Chaza’ mara kwa mara. Hali hii inatokana na ubadilishaji wa sauti zinazokaribiana. Isitoshe, mwalimu huyo alichopeka nazali kabla ya baadhi ya konsonanti, kwa mfano, alisema ‘mbaadaye’ badala ya ‘baadaye’. Massamba (2009) anasema kuwa uchopekaji ni hali ambapo irabu, kiyeyusho au konsonanti huingizwa katika neno hasa pale ambapo misingi ya mfanyiko huu una asili katika L1. Udhaifu huu katika ufundishaji uliwafanya wanafunzi ambao hawakuwa makini kufanya makosa ya hijai katika kazi zao.

Mmoja (10%) kati ya walimu watatu (30%) waliokuwa na shida ya matamshi alikiri kuwa ilikuwa vigumu kwake kuwapa wanafunzi mazoezi ya imla yaliyo na sauti zililizomkanganya kutamka. Kulingana na Nadharia ya Uchanganuzi makosa, mwalimu anapaswa kutambua makosa ya wanafunzi na kuyaainisha ili kuyarekebisha. Hili litawezekana ikiwa mwalimu hafanyi makosa ya matamshi na maendelezo ambayo wanafunzi wake wanafanya. Mwalimu mwingine aliyekuwa na shida ya matamshi alisema, "Wanafunzi wangu wanafahamu vyema kuwa baadhi ya sauti hunikanganya kutamka, kwa hivyo wanahitaji kung'amua ni neno lipi ninalozungumzia kulingana na muktadha. Ninapoona kuwa hawafahamu ninalozungumzia, ninaandika ubaoni." Kauli hii inaonyesha kuwa mwalimu huyu alitarajia wanafunzi wake waweze kutambua sauti ambazo zilimkanganya yeye mwenyewe. Baada ya kuelezea udhaifu wa matamshi ya mwalimu, sehemu ifuatayo imechunguza udhaifu uliojitokeza katika vitabu na vifaa vya kufundishia.

### 4.1.4 Vitabu na Vifaa vya Kufundishia

Jedwali la 4.1 linaonyesha kwamba walimu 4 (40%) walidhihirisha udhaifu wa kutotumia vitabu na vifaa vya kufundisha ipasavyo. Mmoja kati yao alisema kuwa hajawahi kutumia silabasi. Alidai kuwa yeye hufuata vitabu vya kiada kwa sababu walioviandika walizingatia silabasi. Aidha, mwalimu huyo alisema kuwa katika kuandaa maazimio ya kazi, alirejelea tu vitabu vya kiada bila kutumia silabasi.

Silabasi ni muhimu sana katika ufundishaji kwani ni kama dira inayomwongoza mwalimu (Achillah, 2010). Kutotumia silabasi kikamilifu kulifanya baadhi ya walimu kupuuza baadhi ya vipengele katika silabasi kama vile somo la imla.

Isitoshe, mwalimu mmoja (10%) alifundisha somo la imla bila maazimio ya kazi ya muhula wa pili. Alipoulizwa na mtafiti atahakikisha vipi kila somo limefundishwa, alijibu kuwa tayari masomo yote yameangaziwa katika vitabu vya kiada. Utafiti huu ulibaini kuwa walimu 4 (40%) kati ya 10 (10%) wa shule za upili waliegemea vitabu vya kiada kuliko sehemu zingine za mtaala kama vile silabasi na maazimio ya kazi. Kutozingatia silabasi kulifanya baadhi ya walimu kufundisha somo la imla mara moja tu kwa mwaka kwa sababu vitabu vingi vya kiada vimeangazia somo hili mara moja tu. Kando na vitabu na vifaa vya kufundishia, kulikuwa na udhaifu wa maandalizi ya walimu ambao umechunguzwa katika sehemu ifuatayo.

### 4.1.5 Maandalizi ya Walimu

Utafiti uliofanywa nyanjani ulifichua kuwa walimu 5 (50%) kati ya 10 (100%) waliofanyiwa utafiti hawajapata mafunzo mahsusi kuhusu ufundishaji wa somo la imla. Wao walitegemea silabasi na vitabu vya kiada ambavyo vimeeleza kijuujuu jinsi ya kufundisha somo la imla. Walimu 4 (40%) walisema kuwa walijifunza mbinu za kufundishia somo la imla kupitia semina na warsha mbalimbali. Aidha,

walimu wote 6 (60%) waliokuwa na shahada ya kwanza walitoa madai kuwa hawakupokea mafunzo ya kina kuhusu ufundishaji wa somo la imla katika vyuo vikuu, walitegemea masomo ya jumla tu kuhusu mbinu za ufundishaji wa stadi mbalimbali. Walimu 2 (20%) waliosomea diploma walisema kuwa walipata maandalizi ya kufundisha imla japo si ya kina.

Kulingana na misingi ya Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano, mbinu za ufundishaji kama vile matumizi ya lugha mara kwa mara darasani husisitizwa kwa kuwa mtu hufahamu lugha vyema kwa kuitumia. Kwa hivyo, ni vizuri walimu waandaliwe vyema kufunza L2. Walimu waliosema kuwa walikuwa wamehudhuria semina na warsha za kuimarisha ufundishaji wa stadi ya kuandika walikuwa 5 (50%) pekee. Matokeo haya yanadhihirisha kuwa walimu wengi wanafundisha imla bila kupata maandalizi mahsusi na huenda wasifundishe ipasavyo. Aidha, ilibainika kwamba walimu waliopokea maandalizi ya kufundisha somo la imla walikuwa wabunifu zaidi katika mbinu za kufundisha somo la imla.

### 4.1.6 Kutosahihisha Kazi za Wanafunzi

Kati ya vitabu 90 vilivyopitiwa na mtafiti, mazoezi ya imla katika vitabu 20 hayakusahihishwa. Katika vitabu vingine 10, mwalimu alitia tu sahihi bila kuonyesha makosa. Kwa wanafunzi 20 ambao kazi zao hazikusahihishwa, 10 walikiri kuwa walikusanya vitabu lakini vikarejeshwa bila kusahihishwa. Kupitia

mahojiano yasiyo rasmi na wanafunzi, mtafiti alitambua kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuona haja ya kufanya mazoezi ya imla kwa sababu mara nyingi mwalimu wao hakusahihisha kazi zao. Kwa upande wao, walimu walijitetea kuwa kazi nyingi iliwafanya kutosahihisha vitabu vya wanafunzi mara kwa mara.

### 4.1.7 Uteuzi wa Matini

Kulingana na Jedwali la 4.1, walimu wote 10 (100%) waliohojiwa walionyesha udhaifu fulani kuteua matini ya kufundishia somo la imla. Walimu wanapaswa kutumia matini tofauti kufundisha masomo mbalimbali (K.I.E, 2005). Kwa mfano, kifungu cha fasihi simulizi kinaweza kutumiwa kufundisha uakifishaji, utafiti huu ulibaini matini yaliyotumiwa na walimu kufundisha somo la imla. Mtafiti alichunguza mbinu walizotumia walimu kufanikisha matumizi ya matini kutoka sehemu mbalimbali za lugha ya Kiswahili katika ufundishaji wa imla. Jedwali la 4.2 linaonyesha jinsi walimu walivyoteua matini ya kufundishia somo la imla. Mtafiti aliwauliza watafitiwa kutaja na kueleza matini waliyotumia kufundisha imla. Swali hilo lilimsaidia mtafiti kubaini ikiwa kuna udhaifu wowote katika uteuzi wa matini ya kufundishia somo la imla.

**Jedwali la 4.2: Uteuzi wa Matini ya Kufundishia imla**

| Matini | Kwa wingi sana | Kwa wingi | Kwa Uchache | Kwa Uchache sana | Situmii | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Fasihi Simulizi** | 00(00%) | 02(20%) | 05(50%) | 03(30%) | 00(00%) | 10(100%) |
| **Fasihi Andishi** | 00(00%) | 00(00%) | 02(20%) | 04(40%) | 04(40%) | 10(100%) |
| **Sarufi** | 01(10%) | 05(50%) | 03(30%) | 01(10%) | 00(00%) | 10(100%) |
| **Isimu Jamii** | 02(30%) | 04(40%) | 03(30%) | 01(10%) | 00(00%) | 10(100%) |
| **Insha** | 00(00%) | 00(00%) | 00(00%) | 01(10%) | 09(90%) | 10(100%) |
| **Muhtasari** | 00(00%) | 00(00%) | 00(00%) | 01(10%) | 09(90%) | 10(100%) |
| **Ufahamu** | 04(40%) | 04(40%) | 02(20%) | 00(00%) | 00(00%) | 10(100%) |

Tarakimu katika Jedwali la 4.2 zinadhihirisha kuwa, matini kutoka sehemu mbalimbali za lugha na kwa viwango tofauti zilitumiwa na walimu kufundishia somo la imla. Makala ya ufahamu yalitumiwa na walimu wengi (80%) kufundishia imla yakifuatwa na sarufi, Isimu Jamii, Fasihi, muhtasari na insha mtawalia. Matini za insha na muhtasari zilitumiwa mara chache kama asilimia 90 ya walimu ilivyokiri kuwa haitumii matini hayo. Mtafiti alipowahoji walimu zaidi ilibainika kwamba walitumia matini kutoka kwa vifungu vya ufahamu kwenye

vitabu vya kiada kwa sababu matini hizo pekee ndizo zilizowaelekeza kuhusu miktadha mbalimbali na jinsi ya kufundisha somo la imla.

Aidha, walimu waliotumia matini ya sarufi walidai kuwa yalipatikana kwa urahisi katika vitabu vya kiada hivyo basi kuokoa muda wa kutafuta matini. Ijapokuwa walimu walijizatiti kutumia makala kutoka masomo mbalimbali, mtafiti alitambua kwamba takriban asilimia hamsini (50%) ya walimu walitatizika kuteua makala kutoka masomo tofauti ya Kiswahili. Walimu hawa walitoa sababu tofauti kama vile ukosefu wa muda, kutofahamu jinsi ya kuteua makala na ukosefu wa vitabu vya kuteua makala.

Asilimia 50 ya walimu walisema kuwa, iliwabidi kuteua wenyewe vifungu, sentensi na maneno ya kufundishia imla kwa njia mseto; hili halikuwa rahisi kwao kwani walikosa muda wa kutosha. Asilimia 40 ya walimu walisema kuwa, hawakukishughulikia kipengele cha imla kwa upana kwa sababu mada za imla hazikuwa wazi na zimedokezwa kwa kifupi tu katika silabasi. Udhaifu huu ulisababisha walimu hawa kutofundisha somo la imla kwa kina kwa sababu waliegemea tu mbinu na matini waliyopewa kwenye vitabu vya kiada. Quist (2000) anasema kuwa, walimu hupenda kutumia mbinu zilizodokezwa vitabuni kuliko kutumia mbinu walizobuni wao wenyewe. Utafiti huu uligundua kuwa walimu 4 (40%) waliegemea makala ya vitabu vya kiada kinyume na silabasi ya

Kiswahili (KIE, 2005) inavyodokeza kuwa walimu wanaweza kutumia makala kutoka sehemu mbalimbali kama vile magazeti, majarida na vitabu vingine vya darasani.

Walimu waliofunza somo la imla kwa kutumia matini ya isimu jamii na fasihi walisema kuwa masomo hayo ni mapana na yaliwawezesha wanafunzi kufahamu istilahi ngeni kwani yalikuwa bado mageni kwa wanafunzi.  Isitoshe, walimu waliohojiwa walisema kuwa, waliwasomea wanafunzi wao istilahi na kuzifafanua ili wazielewe bali hawakuwa na lengo la kukuza tahajia ya wanafunzi na kuwezesha uakifishaji bora kama yalivyo malengo ya somo la imla. Aidha, hawakudhamiria kukuza vipengele vingine vya lugha katika somo la imla. Data zilizowasilishwa katika Jedwali la 4.2 zinadhihirisha kuwa, kwa jumla walimu walitatizika kutekeleza agizo la K.I.E (2005) la kuseta masomo mbalimbali ya Kiswahili likiwemo somo la imla.

Baada ya kuchunguza udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji wa imla, sehemu ifuatayo imechunguza udhaifu uliojitokezakatika ujifunzaji wa imla.

## 4.2 Udhaifu Uliojitokeza katika Ujifunzaji wa Imla

Sehemu hii imechanganua udhaifu uliojitokeza katika ujifunzaji wa somo la imla. Baadhi ya udhaifu huo ni kama vile matamshi yasiyofaa ya wanafunzi na kutokuwa makini katika somo la imla.

### 4.2.1 Matamshi na Maandishi ya Wanafunzi

Kawoya na Ryanga (2003) wanasema kuwa wanafunzi huandika jinsi wanavyotamka. Mwanafunzi akizoea kutamka kwa usahihi, ataendeleza maneno vizuri katika maandishi. Kati ya kazi 90 zilizopitiwa na mtafiti, wanafunzi 26 waliendeleza baadhi ya maneno visivyo. Kwa mfano, wanafunzi wanne waliandika *anapala* badala ya *anapara*, watano wakaandika *Jaza* badala ya *Chaza*, wawili wakaandika *wacha* badala ya *washa*, watatu wakaandika *bio* badala ya *mbio*. Wilkins (1972) anasema kwamba, makosa kama yale ya sarufi na maendelezo yasiyofaa yanaweza kujidhihirisha katika maandishi ya wanafunzi.

Mtafiti alitambua kuwa baadhi ya wanafunzi huandika maneno wanayotumia sana katika mazungumzo yao, kwa mfano mwanafunzi mmoja aliandika ‘shenji’ badala ya ‘shemeji’ na ‘mapacha’ badala ya ‘pacha’. Walimu waliohojiwa kuhusu suala hili walisema kuwa wanafunzi wengi huandika maneno ambayo wamezoea kuzungumza katika insha zao ama maandishi ya kawaida. Ikiwa maneno hayo

hayana maana kisarufi, basi baadhi ya wanafunzi hao wanafanya makosa katika maandishi. Ilibainika katika utafiti huu kwamba makosa ya matamshi yalipungua walipofanya mazoezi ya mara kwa mara katika sauti zilizowatatiza. Kwa hivyo, wanafunzi hao wakishirikiana na walimu wao na kufanya mazoezi ya kutosha, watapunguza au hata kumaliza makosa ya matamshi yanayojitokeza katika maandishi.

**4.2.2 Kutokuwa Makini katika Somo la Imla**

Wanafunzi 454 kutoka madarasa 10 walichunzwa. Kati yao, 230 (50.7%) walikuwa wasichana na 224 (49.3%) walikuwa wavulana. Baada ya zoezi la darasani, mtafiti aliteua kazi za wanafunzi 90 alizotumia kuchunguza jinsi wanafunzi walivyofanya zoezi la imla. Kupitia upekuzi wa madaftari, mtafiti alitambua kuwa kazi za wanafunzi 20 kati ya 90 hazikuwa zimesahihishwa. Kati ya wanafunzi 20 ambao kazi zao hazikusahihishwa, kumi walikiri kuwa walikusanya madaftari na wengine kumi wakasema hawakukusanya madaftari yao. Mtafiti alipowauliza wanafunzi hao sababu za kutokusanya kazi zao, wanne walisema hawakufahamu kuwa vitabu vilikusanywa na wawili wakasema kuwa hawakukamilisha zoezi kwa sababu hawakuwa darasani somo lilipoanza. Aidha, wanne kati yao walisema kuwa hawakuona umuhimu wowote wa somo hilo kwa hivyo hawakukusanya madaftari. Isitoshe, wanafunzi wengine 5 kati ya 90 waliacha mapengo mengi katika katika zoezi la imla tofauti na mazoezi mengine.

Kupitia upekuzi wa madaftari na majibu ya wanafunzi hawa kuhusu sababu za kutokusanya madaftari yao ya imla, mtafiti alifikia uamuzi kuwa baadhi ya wanafunzi hawakuwa makini katika somo la imla kwa kuwa hawakulichukulia na uzito unaofaa. Aidha, mwanafunzi mwingine aliandika ‘mpunga’ badala ya ‘mkunga’ na ‘alingutuka’ badala ya ‘aligundua’. Utafiti huu ulithibitisha kuwa, huenda mwanafunzi huyu hakuwa makini mwalimu alipokuwa akiwasomea kifungu.

Baada ya kuchunguza udhaifu uliojitokeza katika ujifunzaji wa imla, sehemu ifuatayo imechunguza udhaifu uliojitokeza katika silabasi na vifaa vya kufundishia ili kubaini ikiwa vilikuwa na udhaifu wowote ulioleta changamoto za kufundishia kwa walimu.

### 4.3 Maelekezo ya Silabasi na Vifaa vya Kufundishia

Mtafiti alichunguza silabasi ya Kiswahili na kitabu cha kiada (KLB, 2018) ili kutambua jinsi silabasi hiyo ilivyoelekeza walimu kufundisha somo la imla. Vipengele vilivyoorodheshwa katika silabasi na ambavyo vililenga ufundishaji wa imla vilichunguzwa na mtafiti. Kitabu hicho cha kiada (KLB, 2018) kiliteuliwa kwa sababu ndicho kilichopendekezwa na taasisi ya ukuzaji mitaala (KICD) na kinatumika katika shule zote za upili nchini Kenya. Mtafiti alichunguza lengo,

vifaa, mada na mbinu za kufundishia somo la imla. Kupitia uchunguzi wa silabasi, mtafiti alipata data ambazo zimeonyeshwa katika Jedwali la 4.3.

**Jedwali la 4.3: Jinsi Silabasi inavyoelekeza Ufundishaji wa Imla**

| **Kipengele** | **Jumla** |
|---|---|
| Lengo | 03 |
| Jinsi ya Kufundisha | 01 |
| Tathmini ya Imla | 01 |
| Vifaa vya Kufundishia | 02 |
| Mada za Imla | 00 |

Matokeo katika Jedwali la 4.3 yanadhihirisha kwa, silabasi na kitabu cha kiada (KLB, 2018) haikulipa somo la imla umuhimu wa kutosha kwa kuwa haikutoa orodha ya vipengele vyote vya somo la imla kikamilifu. Kwa mfano, mwongozo wa kitabu cha kiada (KLB, 2018) umedokeza kuwa mwalimu awasomee wanafunzi kifungu huku wakiendeleza bila kuonyesha pahali ambapo kifungu chenyewe kitatoka. Isitoshe, mwongozo huo haujabainisha mada mbalimbali za kufundisha katika somo la imla. Aidha, kitabu hicho kimeonyesha mbinu moja tu ya kufundisha somo la imla. Walimu wengi wanaotegemea silabasi na kitabu cha kiada (KLB, 2018) kwa kiwango kikubwa walionekena kuegemea mbinu hiyo moja iliyodokezwa kwenye silabasi. Matokeo haya yanaonyesha kuwa silabasi na

vitabu vya kiada hazikudokeza mazoezi na mada za kufundishia somo la imla, basi vifaa hivyo havikutoa uelekezi kamilifu kuhusu ufundishaji wa somo la imla.

Baada ya kuchunguza udhaifu katika silabasi na vifaa vya kufundishia, sehemu ifuatayo ndiyo inayohitimisha sura hii.

### 4.4 Hitimisho

Sura hii ililenga kuchunguza udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla. Utafiti huu ulibaini udhaifu katika ufundishaji, ujifunzaji na katika vifaa vya kufundishia Kiswahili. Mtafiti alibaini kuwa, japo kuna udhaifu katika vifaa, silabasi na ujifunzaji wa somo la imla, changamoto nyingi zinatokana na udhaifu katika ufundishaji. Ilibainika katika utafiti huu kuwa wanafunzi wengi wanaendeleza maneno jinsi wanavyotamkiwa na walimu wao hata kama maneno hayo yana makosa. Kwa hivyo, inapasa walimu kuwa makini sana wanapofundisha somo la imla. Sura inayofuata ndiyo inayotutamatishia utafiti huu.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilichunguza udhaifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa imla. Ilibainika kwamba, kuna udhaifu katika ufundishaji wa somo la imla unaoweza kutinga ujifunzaji wa somo hilo. Aidha, baadhi ya wanafunzi walidhihirisha udhaifu katika ujifunzaji wa somo la imla. Sura hii ndiyo inayotamatisha utafiti wetu. Sura yenyewe imeangazia muhtasari wa tasnifu, matokeo ya utafiti, changamoto za utafiti na kutoa mapendekezo ya utafiti huu.

## 5.1 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu umetathmini ufundishaji na ujifunzaji wa imla katika shule za Sekondari. Tasnifu hii ina sura tano. Sehemu ya kwanza imeeleza usuli wa mada, maswali na malengo ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu na nadharia zilizotumika kwa utafiti. Katika sura inayofuata, vipengele vya lugha ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla vimechanganuliwa. Sura ya tatu imechunguza mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha somo la imla na changamoto ambazo walimu hupata wanapofundisha somo hilo. Katika sura ya nne, udhaifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa imla umeelezwa. Sura hii imewasilisha muhtasari wa tasnifu, changamoto katika utafiti, matokeo na mapendekezo ya utafiti huu.

Malengo ya utafiti huu yalikuwa kuchunguza vipengele vya stadi ya kuandika ambavyo wanafunzi hujifundisha katika somo la imla, kueleza mbinu wanazotumia walimu kufundishia somo la imla na changamoto wanazokumbana nazo katika ufundishaji wa somo hilo na kudhihirisha udhaifu unaojitokeza katika ujifunzaji na ufundishaji wa somo la imla ili kupendekeza namna ya kuliboresha. Mihimili ya Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ya Corder (1967) ilitumika kuchanganua vipengele vya lugha ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla. Kulingana na Nadharia hii, makosa ya wanafunzi yanapoangaziwa na kurekebishwa mara kwa mara, mwanafunzi huyo atapata umilisi wa lugha. Mtafiti alichanganua makosa waliyofanya wanafunzi kupitia uchunzaji wa darasani na upekuzi wa vitabu ili kufahamu vipengele vya lugha walivyojifunza katika somo la imla. Nadharia ya Lugha ya Mawasiliano ilichanganua mbinu zinazotumiwa na walimu kufundisha somo la imla na changamoto zinazowakumba wanapofundisha somo hilo. Kulingana na Nadharia hii, wanafunzi wakitumia lugha mara nyingi darasani, watajifunza lugha hiyo vyema. Kupitia mahojiano na walimu na uchunzaji wa darasani, mtafiti alichunguza jinsi walimu walivyofundisha somo la imla na udhaifu uliojitokeza katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo hilo.

Suala la utafiti lilitokana na wanafunzi wengi wa shule za sekondari kuendelea kufanya makosa ya hijai, uakifishaji na sarufi ambayo yanapaswa kupunguzwa au

kuondolewa kabisa na somo la imla. Utafiti huu ulinuia kutoa mapendekezo ya kuboresha somo la imla.

Utafiti huu ulifanywa katika Gatuzi la Trans- Nzoia. Shule 5 zilihusishwa katika utafiti. Aidha, walimu 10 na wanafunzi 454 walishirikishwa katika utafiti huu. Sampuli kusudi ilitumiwa kuteua eneo la utafiti na mbinu bahatishi ikatumiwa kuchagua shule tano baada ya shule hizo kuwekwa kwenye makundi.

### 5.2 Matokeo ya Utafiti

Mbinu za mahojiano, uchunzaji na ukaguzi wa daftari za wanafunzi zilitumika kupata matokeo ya utafiti huu. Data ilipochanganuliwa, baadhi ya mambo yaliyojitokeza na ambayo yana uhusiano na uwasilishaji na upokezi wa somo la imla ni kama yafuatayo:

Sura ya pili ilichanganua vipengele vya lugha ambavyo wanafunzi hujifunza katika somo la imla. Ilibainika kuwa wanafunzi walijifunza uendelezaji sahihi wa maneno, uakifishaji bora, hati nadhifu, kuwa makini, msamiati mpya na sarufi sahihi katika somo la imla. Kwa sababu ya umuhimu wa somo la imla katika stadi za kuandika na kuzungumza, somo hili linapaswa kutiliwa maanani zaidi na walimu na wanafunzi.

Sura ya tatu ilitathmini mbinu wanazotumia walimu kufundisha somo la imla na changamoto wanazokumbana nazo katika ufundishaji wa somo hilo. Iliibuka kuwa walimu 9 (90%) kati ya 10 (100%) walitumia mbinu moja tu kufundishia somo la imla. Walimu waliotumia mbinu hii walidai kuwa vitabu vya kiada viliwaelekeza kutumia mbinu hiyo bali sio kwa sababu iliwapa matokeo mazuri. Hali hii ilielezwa kama iliyokuwa ikichangia ukosefu wa motisha kwa wanafunzi katika somo la imla. Baadhi ya wanafunzi waliona somo hilo kama njia ya mwalimu kutamka haraka na kuwatafutia makosa ya uendelezaji wa maneno. Mbinu nyingine zilizotumiwa na walimu ni kama vile mwanafunzi mmoja kuwasomea wengine darasani au kwenye vikundi na matumizi ya tepurekoda.

Isitoshe, iliibuka katika sura ya tatu kuwa walimu walipata matatizo kadhaa walipokuwa wakifundisha somo la imla. Changamoto zilizojitokeza katika utafiti huu ni kama vile ukosefu wa muda, idadi kubwa ya wanafunzi, ufundishaji wa njia mseto, tatizo la uteuzi wa matini na mazoezi ya kutathmini wanafunzi. Walimu waliotaja changamoto ya ukosefu wa muda wa kutosha kufundisha somo la imla walidai kuwa silabasi ya Kiswahili ilikuwa pana sana. Kando na kuwa na vipengele vingi vya kufundishwa, silabasi hiyo haikuweka wazi maelekezo ya jinsi ya kufundisha somo la imla.   Isitoshe, walimu walidai kuwa, walikuwa na ugumu wa kupata muda wa kufundisha imla na iliwabidi walifundishe kwa njia mseto na

masomo mengine kama sauti tatanishi. Mwisho, walimu waliohojiwa walidai kuwa, walitatizika kuseta somo la imla na masomo mengine kama vile sarufi.

Sura ya nne ilichunguza udhaifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la imla. Mtafiti alibaini kuwa, nafasi ya somo la imla katika silabasi na vitabu vya kiada imedunishwa hivyo basi baadhi ya walimu hawakujiandaa ipasavyo kulifundisha. Kwa ujumla, silabasi haikueleza kwa upana na uwazi jinsi ya kufundisha somo la imla. Aidha, silabasi hiyo haikudhihirisha mada na mazoezi yanayoweza kufanywa na wanafunzi katika somo la imla.  Isitoshe, silabasi haikutengea somo la imla muda wa kutosha wa kufundisha. Udhaifu mwingine ulijitokeza katika matini ya kufundishia. Iliibuka kuwa matini zilizotumiwa kwa wingi kufundishia somo la imla zilikuwa zile zilizodokezwa kwenye vitabu vya kiada hasa vifungu vya ufahamu. Walimu wengi (50%) walitumia kwa uchache matini mengine kama yale ya fasihi, sarufi, isimu jamii na muhtasari. Kwa hivyo, ufundishaji wa njia mseto haukuzingatiwa kwa ukamilifu kama vile silabasi ya K.I.E (2005) inavyoeleza. Ilibainika kuwa, baadhi ya walimu na wanafunzi walikuwa na udhaifu mbalimbali uliosababisha changamoto kuu na hata kutinga ufundishaji wa imla. Udhaifu huo ulijitokeza katika maandalizi ya walimu, silabasi, athari ya L1 na katika mbinu za kufundishia somo la imla.

## 5.3 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kadhaa licha ya kufaulu kwa kiasi kikubwa. Kwanza, matini nyingi zinazohusisha imla zimeandikwa kwa Kimombo. Kwa hivyo, ilimbidi mtafiti kutafsiri mara kwa mara taarifa mbalimbali zilipohitajika: hili lilimgharimu mtafiti pesa na muda mrefu. Aidha, tafiti zinazohusiana na somo la imla ni chache, kwa hivyo kulikuwa na changamoto ya matini ya kurejelewa na mtafiti. Katika shule za kitaifa na zile za kimkoa, walimu walikuwa na dhana ya kupotezewa muda wakati wa vipindi vya kawaida. Ilimbidi mtafiti kubadilisha ratiba yake na kufanya utafiti wakati wa jioni katika shule hizo.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Wanafunzi wengi watanufaika kupitia utafiti huu kwa sababu umetambulisha makosa ya kuendeleza maneno wanayofanya wanapojifunza Kiswahili. Hivyo basi, wanafunzi watafaidika kwa ushauri watakaopata kutoka kwa walimu wao. Hii ni baada ya walimu kufuata mapendekezo ya mtafiti kuhusu jinsi ya kutatua makosa ya tahajia ya wanafunzi. Isitoshe, walimu wataweza kuboresha jinsi ya kufundisha Kiswahili na kuwawezesha wanafunzi wao kupita mitihani. Mwisho, walimu watatambua jinsi ya kupunguza na kuondoa makosa katika maandishi. Wanaoandika vitabu vya kiada vya Kiswahili watafaidika wakifahamu visababishi vya makosa mbalimbali ya wanafunzi ili watoe mazoezi yatakayokabiliana na makosa ambayo yamedhihirishwa katika utafiti huu.

## 5.5 Mapendekezo

Mtafiti anapendekeza yafuatayo kwa kuzingatia matokeo ya utafiti: Kwa kuwa somo la imla linakuza kwa kiasi kikubwa vipengele vingi vya stadi ya kuandika, wanafunzi wanapaswa kuhamasishwa na walimu wao kuhusu somo la imla. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi watajifundisha na kujielekeza wenyewe na linalowatatiza wampelekee mwalimu. Isitoshe, mazoezi hayo yatakuza uelewa wa wanafunzi wa vipengele tofauti vya stadi ya kuandika na kuzungumza.

Pili, walimu wanapaswa kuelekezwa kuhusu mbinu mbalimbali za kufundishia somo la imla kupitia warsha na semina za Kiswahili. Warsha hizo zitawasaidia walimu kuwa wabunifu zaidi na kubuni mbinu tofauti za kufundishia somo la imla kwa sababu vitabu vya kiada vinapendekeza mbinu moja pekee.

Tatu, walimu wote waliohojiwa walionekana kutatizika kupata matini ya kufundishia somo la imla. Wengi walitumia makala yaliyopendekezwa kwenye vitabu vya kiada. Ili kutatua tatizo hili, matini mengine yanapaswa kubuniwa kutoka masomo tofauti lakini yanayolenga kufundishia somo la imla. Aidha, masomo ya imla yanayopaswa kufundishwa kwa kutumia matini hizo yadhihirishwe ili yashughulikiwe kwa undani. Ili kutimiza mapendekezo haya, vipindi maalum vinapaswa kutengwa kufundisha somo la imla.

Nne, ili kuondoa tatizo la walimu kuegemea mbinu moja pekee ya kufundisha somo la imla na kutoshirikisha mbinu nyingine, mtafiti anapendekeza walimu wahamasishwe jinsi ya kutumia mbinu nyinginezo za kufundisha imla. Mbali na mbinu ya mwalimu kusoma huku wanafunzi wakiendeleza, walimu wanapaswa kutumia mazoezi mengine kuhakikisha kuwa wanafunzi wamejifunza vipengele vya lugha walivyokusudiwa kujifunza. Isitoshe, vitabu vya kiada vinapaswa kuweka wazi mazoezi mengine ambayo walimu wanaweza kutumia kufanikisha somo la imla.

Ile kuweza kuondoa changamoto nyingine kama vile; kufundisha kwa njia mseto, ukosefu wa muda, idadi kubwa ya wanafunzi na changamoto zinazohusisha matini na tathmini, mtafiti anapendekeza kuwa, washikadau wa elimu waandae warsha na semina za Kiswahili ili waweze kuwahamasisha walimu jinsi ya kufundisha somo la imla kwa njia mseto. Pili, walimu wahamasishwe kutengea somo la imla vipindi maalum vya kufundisha kama ilivyoelekezwa katika silabasi ya K.I.E (2005). Isitoshe, Taasisi ya Ukuzaji Mitalaa (K.I.C.D) iongeze vipindi vya kufundisha Kiswahili kutoka 6 hadi 8 kwa juma ili vipengele vyote vya lugha vishughulikiwe ipasavyo. Tatu, matini za kufundishia somo la imla zibainishwe waziwazi. Kuongeza kwa hayo, silabasi ya Kiswahili ifanyiwe marekebisho ili somo la imla lipewe umuhimu unaofaa kwa kubainisha mazoezi na mbinu ya kufundisha somo hilo. Ili kukabiliana na tatizo la idadi kubwa ya wanafunzi, utafiti huu

unapendekeza kuwa, tume ya kuwaajiri walimu (T.S.C) iwaajiri walimu zaidi wa Kiswahili. Kando na kuajiri walimu zaidi, walimu wa somo la Kiswahili wafundishe Kiswahili lugha na fasihi wala si Kiswahili na somo lingine. Ufundishaji wa Kiswahili pekee utawawezesha walimu kuzamia vipengele vyote vya stadi ya kuandika na hata kupata muda wa kusahihisha kazi za wanafunzi. Mwisho, kutokana na changamoto ya tathmini inayofanya baadhi ya walimu kutotilia maanani somo la imla, utafiti huu unapendekeza imla kutahiniwa katika mtihani wa kitaifa. Aidha, vitabu vya kiada vifanyiwe marekebisho ili vibainishe mazoezi tofauti ya kutathmini wanafunzi darasani.

Utafiti mwingine wa namna hii unaweza kutekelezwa katika viwango vya chini vya elimu ili kuweka wazi kile wanafunzi wanachojifunza na kuonyesha matatizo yanayojitokeza wanapojifunza imla na kisha kutoa mapendekezo mwafaka. Utafiti mwingine unapaswa kufanywa katika vyuo vikuu ili kuchunguza jinsi walimu wanavyoandaliwa kufundisha stadi ya kuandika katika shule za sekondari. Aidha, utafiti mwingine wa imla unaweza kufanywa kwenye shule za sekondari ili kuthibitisha ikiwa somo hilo linaboresha matokeo ya lugha ya Kiswahili. Mwisho, vitabu vya kiada vya Kiswahili vinapaswa kuchunguzwa ili kubaini ikiwa vinajitosheleza katika kuwaongoza walimu kufundisha somo la imla.

## MAREJELEO


Achilah, A. R. (2010). *Matumizi ya Mbinu ya Kimuktadha katika Ufundishaji wa Msamiati wa Kiswahili katika Shule za Upili za Wilaya ya Kakamega*. Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Masinde Muliro. Kakamega.

Alimatul, A. 2019). *The Effect of Dictation Method on the Students Listening Skill among the Eleventh Grader at Ma Ma'arif 1, Punggur*. Unpublished Undergraduate Thesis. State Institute for Islamic Studies of Metro. Indonesia.

Benaars, G.A., Otiende, J.E. & Boisvert, R. (Eds) (1994). *Theory and Practice of Education*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Bishop, G. (1985). *Curriculum Development: A Textbook for Students*. London: Macmillan Education Limited.

Bowen, T. (2000). Methodology. *Using Dictation in Language Teaching*. Macmillan Education Group.

Cooper, J.P. (1991). *Speech Communication for the Classroom Teacher.* Gorsuch Scarisbrick Publishers, Arizona, Scottsdale.

Corder, S.P (1967). The Significance of Learners Errors: *International Review of Applied Linguistics*. Vol. 5.

Corder, S. P. (1971). *Idiosyntactic Dialects and Error Analysis*, IRAL, Vol. 9:149-159.

Corder, S. P (1973). *Introducing Applied Linguistics*. Middlesex: Penguin. (1974).

Corder, S. P. (1974). *Error Analysis* in J. Allen and S. Corder (eds). Vol. 3. Oxford University Press.

Davis, P & Rinvolucri, M. (1988). *Dictation: New Methods, New Possibilities*. Cambrige: Cambridge University Press.

Ellis, R. (1997). *Second Language Acquisition*. Oxford: Oxford University Press.

Fischer, S.R. (2003). *A History of Writing.* London: Reaktion Books.

Fisher, C. M (2001). *Dictation: What and How Students Learn from it*. MA Thesis, Brattleboro International Training School, Vermont.

Frodesen, J. (1991). Grammar in Writing. *In Teaching English as a Second or Foreign Language,* M. Celce- Murcia. (Ed) Pp. 268. Boston: Heinle & Heinle Publishers.

Gakuo, J. (2014). *Changamoto za Uchanganuzi na Ufasiri wa Ushairi katika Shule za Upili Nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamifu ambayo Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Halliday, M. (1964). *The Linguistic Science and Language Teaching*. London: Longman.

Hawes, H. (1979). *Curriculum and Reality in the African Primary School*. London: Longman.

Hymes, D. (1971). *On Communicative Competence*. Philadelphia: University of Pennsylvania Press.

Johnson, K. (1982). *Communicative Syllabus Design and Methodology*. Oxford: Pergamon Institute of English.

Kamal, A. (2005). *Teaching of the Development of Written English in Primary and Junior Secondary School*s. A paper Presented at the Diagnostic Workshop for Teachers of English Organized by State Universal Basic Education (SUBEB), Jigawa, Nigeria.

Karingi, W. (2012). *Ufunzaji wa Vivumishi na Vibainishi katika Shule za Upili Wilayani Kirinyaga: Mtazamo wa Sintaksia Finyizi*. Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

Kawoya, V. na Ryanga, C. (2003). ECT 313: *Mbinu za Lugha na Fasihi.* Institute of Open Learning. Kenyatta University.

Kenya Institute of Education (2005). *Secondary Education Syllabus*. Nairobi: Author.

Kenya Literature Bureau (2018). *Kiswahili Kitukuzwe Kidato cha Pili*. Nairobi: Author.

Kombo, D.K. & Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction.* Nairobi: Paulines Publications Africa.

Massamba, D.P.B. (2009). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: TUKI.

Mason, C. (2012). Dictation for Teaching English. Retrieved on 22/10/2021.www.google.com

Mbaabu, I. (1985). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

McDonough, J. & Shaw, C. (1993). *Materials and Methods in ELT: A Teachers Guide.* Oxford: Blackwell.

Milroy, L. (1987). *Observing and Analyzing Natural Language. A Critical Account of Sociolinguistic Method*. Oxford: Basil Blackwell.

Mugenda, O. & Mugenda, A. (2019). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Kenya Act Press.

Mulwa, N. (2014). *Fonolojia ya Nomino Mkopo za Kikamba kutoka Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili ambayo Haijachapishwa. Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Musau, P. (1993). *Aspects of Interphonology. The Study of Kenyan Learners Swahili*. Bayrenth: Bayrenth African Study.

Musau, P. na Chacha, L. (2001). *Mbinu za Kisasa za Kufundishia Kiswahili. Kwa Walimu wa Shule za Msingi, Upili na Vyuo*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mutiga, J. (2008). Nature and Nurture: Tenets in the Acquisition of Kiswahili as a Second Language in the Kenyan Bilingual System of Education. In Ogechi, N. et al. (Eds.), *Nadharia Katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika* (pp. 397-405). Moi University.

Natalicio, D. S. (1979). Repetition and Dictation as Language Testing Techniques. *Modern Language Journal*, 63(4), 165-176.

Ndalu, A., Babusa, H. na Mirikau, S. (2014). *Kamusi Teule ya Kiswahili Sanifu.* Nairobi: East African Education Publishers Ltd.

Nganje, D. na Njogu, K. (2008). *Kiswahili kwa Vyuo vya Ualimu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ngugi, B. (2008). *Tathmini ya Mtalaa wa Isimujamii wa Shule za Upili Nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Norrish, J. (1983). *Language Learners and their Errors*. London: Macmillan Press.

Odeo, I. na Maina G. (2008). *Fani ya Isimujamii kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Oxford University Press.

Odeo, I., Simiyu, A., & Mukwa, C. (2008). Oral Questioning in the Pedagogy of Kiswahili Grammar in Secondary Schools in Kenya. *Journal of Science, Technology, Education & Management (J-STEM) of MMUST*. Vol 2, Pp.134-135.

Okoba, B. (2008). *Kuchunguza Ufundishaji wa Kusoma kwa Sauti katika Madarasa ya Kwanza, Pili na Tatu katika Shule za Msingi.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa)

Oller, J. (1971). Dictation as a Device for Testing Foregn Language Proficiency: *English Language Teaching,* vol. 25, no. 3, pp. 254-259.

Oller, J. & Streiff, V. (1975). Dictation: A Test of Grammar-Based Expectations. *English Language Teaching Journal,* vol. 30, no.1, pp. 25-36.

Onyango, J. (1990). *Mielekeo ya Wasomi kuhusu Matumizi ya Kiswahili Nchini Kenya.* Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi. (Haijachapishwa)

Orodho, A. (2003). *Essentials of Educational and Social Science Research Methods.* Nairobi: Masola.

Powell, B. (2009). *Writing: Theory and History of the Technology of Civilization*. Oxford: Blackwell.

Quist, D. (2000). *Primary Teaching Methods.* London, Macmillan Education Ltd.

Richards, J. & Rodgers, S. (1986). *Approaches and Methods in Language Teaching.* Cambridge: Cambridge University Press.

Roper, E. (1989). *Difficulties I Encountered with the Writing of Post Graduate Students*. The Independent Magazine. 24th June, 1989.

Sarki, M. (2015). *Effects of Dictation on the Written English of Junior Secondary School Students in Jigawa State*.Unpublished Masters Thesis. Ahmadu Bello University, Nigeria.

Safri, M. (2011). Correlation between Dictation Ability and Writing Ability. Retrieved on 20.10.2021 from www.google.com.

Seliger, W. & Shohamy, E. (1989). *Curriculum Theory and Practice in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

Shiundu, J. & Omulando, J. (1992). *Curriculum Theory and Practice in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press.

TATAKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Toleo la Pili: Nairobi: Oxford University Press.

Wamitila, W. (2016). *Kamusi pevu ya Kiswahili*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wanyoike, E. (1978). Vikwazo katika Mafunzo ya Kiswahili Nchini Kenya. *Lugha Journal for Language Teachers in Kenya*. Nairobi, vol. 5, pp. 35-42.

Willis, J. & Willis, D. (1996). *Challenge and Change in Language Teaching*. Oxford: Heinemann.

## KIAMBATISHO A: KIONGOZI CHA MAHOJIANO KWA WALIMU

1. Jina la shule
2. Aina ya shule. Kitaifa ( ) Kaunti ( ) Kaunti ndogo ( )
3. Kiwango cha juu cha elimu: Stashahada ( ) Shahada ( ) Uzamili ( ) Uzamifu( )
4. a) Unatumia mazoezi yapi kufundisha na kuimarisha stadi ya kuandika?

   b) Unatazamia wanafunzi wako kujifunza nini katika mazoezi hayo?

   c) Ni mazoezi ya somo lipi yanayoboresha stadi ya Kuandika zaidi na unawapa wanafunzi mara ngapi kwa muhula?
5. Unatumia mbinu gani kutambua makosa katika lugha andishi na kuyarekebisha?
6. Unafikiri ni nini kinachoweza kuathiri stadi za kuongea na kuandika kwa mwanafunzi?
7. Ni changamoto zipi unazopata unapofundisha somo la imla?
8. Unatumia mbinu zipi kufundishia somo la imla?

## KIAMBATISHO B: KIONGOZI CHA UCHUNZAJI

1. Mwalimu anatumia mbinu zipi kufundisha somo la imla?
2. Ni matini gani zinazotumiwa na ni za kiwango kipi?
3. Kasi ya mwalimu anaposoma. Haraka (  ) Kadri (  ) Polepole (  )
4. Wanafunzi wanajifunza nini katika zoezi la imla?
5. Ni changamoto zipi zinazojitokeza mwalimu anapofundisha imla?
6. Udhaifu upi unaodhihirika mwalimu anapofundisha imla?

## KIAMBATISHO C: KIFUNGU CHA IMLA

*Shemeji yake Chaza alikuwa mja mzito. Siku moja alipokuwa akipara samaki wa maji ya bara alihisi kizunguzungu. Chaza alipomwona akiwewesuka alikimbia na kumshika. Hali aliyokuwa nayo hakuweza kuachika.*

*Mama naye alifika hima. Ingawa alikuwa amechoka kwa mzigo wa kuni kichwani na shoka zito mkononi, aliviangusha na kuwakimbilia. Walimlaza chali na kumpepea kwa shali waliyoifungua kutoka kichwani pa Chaza. Kisha daktari alifika. Alipotaka kufungua kisanduku chake cha dawa, aligundua kuwa alisahau kicha chake cha funguo nyumbani. Wacha atoke mbio. Aliwasha gari na kuliendesha kwa kasi. Mara mkunga akafika haraka.*

*Hatimaye, dada alinipasha habari kuwa wifi yake Chaza alijifungua watoto pacha. Wanakijiji wote walifurahi.*

# KIAMBATISHO D: BARUA YA SHULE YA KUIDHINISHA UTAFITI

KENYATTA UNIVERSITY
GRADUATE SCHOOL

E-mail: dean-graduate@ku.ac.ke
Website: www.ku.ac.ke

P.O. Box 43844, 00100
NAIROBI, KENYA
Tel. 810901 Ext. 4150

Internal Memo

FROM: Dean, Graduate School

DATE: 26th February, 2019

TO: Kurema Aoko Lonah
C/o Kiswahili Dept.

REF: C50/CE/28517/2013

**SUBJECT: APPROVAL OF RESEARCH PROPOSAL**

We acknowledge receipt of your revised Research Proposal as per our recommendations raised by the Graduate School Board of 9th January, 2019 entitled **"Tathmini ya uwasilishaji na upokezi wa somo la imla katika shule za upili: Gatuzi la Trans-nzoia, Kenya".**

You may now proceed with your Data Collection, Subject to Clearance with Director General, National Commission for Science, Technology and Innovation.

As you embark on your data collection, please note that you will be required to submit to Graduate School completed Supervision Tracking Forms per semester. The form has been developed to replace the Progress Report Forms. The Supervision Tracking Forms are available at the University's Website under Graduate School webpage downloads.

Thank you.

HARRIET ISABOKE
FOR: DEAN, GRADUATE SCHOOL

C.c. Chairman, Department of Kiswahili

Supervisors:

1. Dr. Miriam Osore
   C/o Department of Kiswahili
   Kenyatta University

2. Dr. Leonard Chacha Mwita
   C/o Department of Kiswahili
   Kenyatta University

*HI/ik*

# KIAMBATISHO E: KIBALI CHA NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **195136**

Date of Issue: **07/November/2019**

## RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Ms.. LONAH KUREMA of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Transnzoia on the topic: TATHMINI YA UWASILISHAJI NA UPOKEZI WA SOMO LA IMLA KATIKA SHULE ZA SEKONDARI NCHINI KENYA for the period ending : 07/November/2020.**

License No: **NACOSTI/P/19/2523**

195136

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013

The Grant of Research Licenses is Guided by the Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

CONDITIONS

1. The License is valid for the proposed research, location and specified period
2. The License any rights thereunder are non-transferable
3. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research
4. Excavation, filming and collection of specimens are subject to further necessary clearence from relevant Government Agencies
5. The License does not give authority to tranfer research materials
6. NACOSTI may monitor and evaluate the licensed research project
7. The Licensee shall submit one hard copy and upload a soft copy of their final report (thesis) within one of completion of the research
8. NACOSTI reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice

National Commission for Science, Technology and Innovation
off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623, 00100 Nairobi, KENYA
Land line: 020 4007000, 020 2241349, 020 3310571, 020 8001077
Mobile: 0713 788 787 / 0735 404 245
E-mail: dg@nacosti.go.ke / registry@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke